# Nipashe

Alhamisi Mei 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580225

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Adaiwa kuua mama kwa panga kisa ugumu maisha

UK. 3




UKURASA 11

# Mbunge CCM mbaroni kwa tuhuma ujangili

**POLISI** wadai kunasa chumbani kwake bunduki 16 na risasi 536, nyama inayodhaniwa ya wanyamapori kilo 35 pia...*Endelea ukurasa 2*



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, akionyesha silaha 16 na risasi 536, kwa waandishi wa habari jana, ambazo zinadaiwa kukutwa kwa Mbunge wa Kishapu, Suleiman Masoud Nchambi (picha ndogo), pamoja na nyara za serikali. **PICHA: MARCO MADUHU**

## BAA LA CORONA



Barakoa za vitambaa zinaweza kuleta maambukizo ya Covid-19 kwa mtu kama haitavaliwa kwa usahihi, kushikwa na mikono michafu na kuvaliwa tena kwenye mdomo na pua. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## MBOWE: WAKAIDI WATAVUNA UKAIDI WAO

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


# Ndugai aagiza wabunge watoro warejeshe posho

Makonda atoa saa 24 wakamatwe Dar *UK. 2, 7*


**MICHEZO** YANGA YAANDAA MAMBO MAZURI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mwanafunzi wa darasa la tano, Aristidia Bosco (17) ambaye anasumbiliwa na uvimbe mkubwa kwenye goti lake la mguu wa kulia kwa mwaka mmoja sasa, akiwa na mama yake, katika Mtaa wa Nenetwa, Nyamanoro, wilayani Ilemela, jijini Mwanza jana, akiomba msaada wa fedha kwa Watanzania na serikali, kwa ajili ya kupata matibabu katika Hospitali ya Rufani Bugando, aweze kupona na kuendelea masomo ili kutimizi ndoto zake. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Mbunge CCM mbaroni tuhuma ujangili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia Mbunge wa Kishapu, Seleman Nchambi, kwa tuhuma za kukutwa na silaha na nyara za serikali nyumbani kwake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, mbunge huyo anadaiwa kukutwa na nyara za serikali zilitokana na uwindaji haramu kwenye eneo la Negezi wilayani Kishapu, huku gari lenye namba za usajili T 760 DSD Nissani Hardbody likidaiwa kutumika kwa shughuli hiyo.

Alisema mbunge huyo alikamatwa Mei 3 mwaka huu saa 5:45 usiku, akiwa nyumbani kwake, Mtaa wa Lubaga mjini Shinyanga.

Kamanda Magiligimba alisema kikosi kazi cha askari wa upelelezi wa makosa ya jinai wakiongozwa na David Msangi, wakiwa na ofisa wanyamapori, Perfect Mbwambo, walimkata mbunge huyo nyumbani kwake akiwa na nyara za serikali pamoja na silaha.

"Walipofanya upekuzi nyumbani kwa mbunge huyo, walifanikiwa kukamata nyama inayodhaniwa kuwa ni ya wanyamapori yenye uzito wa kilogram 35 zikiwa zimehifadhiwa kwenye jokofu lililokuwa jikoni na nyingine sehemu ya mazoezi pamoja na kwenye gari, na katika gari hilo, ilikutwa silaha Shotgun yenye namba 46092.

"Katika chumba chake cha kulala, zilipatikana silaha zingine 15 ambazo ni Tzcar 87342, aina ya Air Gun, Tzcar 63729 Rifle, Tzcar 77325, Rifle, Tzcar 87636 Markiv, Tzcar 65673 Rifle, Tzcar 72731 Rifle.

"Tzcar 87342 Airgun, Tzcar 53933 Rifle, Airgun Cz 455 Rifle, Cz 537-2 Rifle, 978836-Mod 151 Shotgun, Pistol aina ya Browning 061738, na kufanya jumla ya silaha zilizokamtwa kuwa 16 na risasi 536 zikiwa kwenye kabati la nguo," alisema.

Magiligimba alisema baada ya uchunguzi kufanyika, waligundua silaha 10 kati ya 16 anazimiliki isivyo halali na kwamba sampuli za nyama wamezipeleka kwenye Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi zaidi.

Alisema upelelezi ukikamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili, huku akitoa onyo kwa yeyote wanaojihusisha na vitendo vya kumiliki silaha isivyo halali.

# Makonda aagiza wabunge watoro wakamatwe Dar

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametoa saa 24 kuanzia jana asubuhi kwa wabunge walioko jijini humo kuondoka, vinginevyo watakamatwa kama inavyofanyika kwa makundi mengine wanayopambananayo, yakiwamo yanayojishughulisha na biashara ya ngono.

Makonda alitoa muda huo, akidai kuwa wabunge kwa sasa wanapaswa kuwa Makao Makuu ya nchi, Dodoma kushiriki vikao vya Bunge la Bajeti, hivyo yeyote atakayeonekana Dar es Salaam, atakamatwa kwa kosa la uzururaji kama wanavyofanya kwa machangudoa.

Makonda alisema mbunge anayepaswa kubaki Dar es Salaam ni yule mwenye kibali kutoka kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai.

"Asiyekuwa na kibali, huyo ni mzururaji kama wazururaji wengine. Kipindi hiki ni hatari na tunawataka watu wanaotoka nyumbani ni wale wanaofanya kazi, hatujaalika wazururaji kutoka mkoani kuja kuzurura.

"Inawezekana wakahatarisha zaidi maisha ya wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwaambukiza corona," alisema.

Makonda alisema kipindi hiki ni muhimu katika Bunge cha wabunge kujadili bajeti na kuwezesha upatikanaji wa mahitaji ya wananchi.

"Wanahitaji barabara, wanahitaji maji, umeme, wanayo mahitaji mengi ndiyo maana walimchagua muende Dodoma kupigania mahitaji yao na wala siyo kuzurura," alisema.

Makonda alidai wabunge wengi wametoka kwenye shughuli yao muhimu waliyochaguliwa kuifanya na kwenda wazururaji Dar es Salaam na wengi wao siyo wakazi wa jiji hilo.

"Saa 24 baada ya hapo tusilaumiane, tutakukamata kama tunavyokamata machangudoa wanaozurura usiku," Makonda alionya.

Kutokana na kauli hiyo, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alimjibu Makonda akisema: "Sitakwenda Dodoma. Nitakaa Dar es Salaam kwa uhuru kabisa.

"Najilinda dhidi ya corona mimi binafsi na familia yangu. Ninakaa nyumbani. Ninawalinda wapigakura wangu wa Kigoma Mjini pia. Hizi saa 24 alizotoa Mkuu wa Mkoa ziishe kwa wabunge, ni... (alitumika neno kali), aniguse, athubutu.

"Mimi ni Mbunge wa Kigoma Mjini. Nipo Dar es Salaam, sijakwenda Dodoma bungeni kwa sababu ninaamini kuwa Bunge lilipaswa kuahirishwa ili kupambana na corona.

"Sitakwenda Dodoma. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam hana mamlaka yoyote ya kuniamulia niwe wapi katika Jamhuri ya Muungano."

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kupitia msemaji wake, Tumaini Makene, kilisema hakiwezi kujibu kauli iliyotolewa na Makonda kwa kuwa yapo mambo mengi ya msingi ya kuyafanyiwa kazi kuliko kauli hiyo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Chadema kupitia kwa Mwenyekiti wake Taifa, Freeman Mbowe, iliwataka wabunge wake kujitenga kwa siku 14 na kutofika eneo lolote la Bunge Dodoma na Dar es Salaam, ingawa baadhi yao wamelikiuka na kuonekana bungeni.

# Bajeti Kuu kujadiliwa siku mbili

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BAJETI Kuu ya Serikali sasa itajadiliwa kwa siku mbili badala ya siku sita hadi saba kama ilivyokuwa miaka mingine.

Ratiba mpya ya shughuli za kikao cha 19 cha Bunge la 11 iliyotolewa jijini hapa, imeonyesha.

Awali, ratiba ilionyesha kuwa bajeti hiyo ingesomwa Mei 29, mwaka huu na kujadiliwa kwa siku sita na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli, kufunga Bunge Juni 30.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo mpya Rais atafunga Bunge Mei 29, mwaka huu.

Ratiba ilionyesha pia kuwa Bajeti Kuu itawasilishwa bungeni Jumatano Mei 20, majira ya saa 10 jioni na mjadala kufanyia Mei 21 na 22.

Vile vile, tofauti na miaka mingine tangu kuanza kwa Bunge la 19, Mei 20, wabunge wataingia mara mbili bungeni, wakati wa asubuhi saa 4:30 na saa 10:00 jioni.

Kutokana na ratiba hiyo kwa sasa kila wizara itafanya mawasilisho yake, mjadala na kupitishwa kwa siku moja na vikao vitaanza saa 8:00 mchana hadi saa 12 jioni.

Mabadiliko hayo yalianza Aprili 20, mwaka huu, lengo ni kuwezesha shughuli kumalizika mapema zaidi.

Pia, baada ya kupitishwa kwa bajeti kuu wabunge watakwenda kwenye mapumziko ya Sikukuu ya Eid, na kurudi Mei 26, kuendelea na miswada mbalimbali.

Miswada inayotarajiwa kuwasilishwa na kujadiliwa katika Bunge hilo ni wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2020, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2020.

Mingine ni Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea wa mwaka 2020, Muswada wa Sheria ya kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu wa mwaka 2020 na Azimio la kuridhia mkataba wa kimataifa wa utoaji mafunzo na vyeti vya wafanyakazi meli za uvuvi wa mwaka 1995.

Baada ya shughuli hizo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), zitafuata na Waziri Mkuu atahutubia na Rais kulifunga Bunge.

Hadi sasa wizara zilizobaki ni ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati, Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Fedha na Mipango.

## HABARI KITAIFA

# SCCUT yapongeza vyama kufutwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SIKU moja baada ya serikali kuvifuta rasmi vyama hewa vya ushirika 3,348, Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT Ltd-1992), kimesema vyama hivyo vilianzishwa kwa malengo ya kisiasa na havikuwa na uhakika wa uhai wake.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa SCCULT Ltd, Hassani Mnyone, akizungumzia uamuzi huo alisema chama hicho kinaunga mkono uamuzi huo wa serikali, kwa vile kulikuwa na makosa yalifanyika wakati wa uandikishaji wa vyama hivyo.

Kwa mujibu wa Mnyone, miongoni mwa makosa hayo ni pamoja na kutozingatiwa kwa hali ya kiuchumi ya muda mrefu ya vyama, jambo ambalo ni muhimu kupima uhai wa chama cha ushirika kuendelea kutoa huduma zake.

"Kimsingi ilikuwa ni muhimu kufanyika, kwa sababu kulikuwa na vyama vingi ambavyo vilikuwa havifanyi kazi yoyote na havijulikani vilipo. Kwa upande wa Saccos ilikuwa ni lazima ifanyike hivyo ili kuhakikisha utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na kanuni zake za mwaka 2019.

"Tunakuwa na Sacco's ambazo tayari zina nguvu na zinahudumia wanachama wake vizuri, sasa hivi tunavyo vyama ambavyo ni hai, vina nguvu na vina hudumia watu wake. Jukumu letu kama wadau ni kuhakikisha vyama hivi vinaendelea kuwa imara kwa kutoa usaidizi mkubwa wa kitaalamu, kuvipatia nafasi ya kujifunza kuanzia wanachama, viongozi na watendaji."

Juzi, Waziri wa Kilimo, Josephat Hasunga, akiwa jijini Dodoma alitangaza kufutwa kwa vyama hivyo vya ushirika, pia alivitaka vyama vilivyosalia kuimarisha mwenendo wao.




Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Azza Hilali (kulia), akitoa msaada wa ngao za uso kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, kuwakinga na maambukizo ya virusi vya corona. Pia alitoa viti vitano kwa ajili ya ofisi ya Klabu ya Waandishi wa Habari wa mkoa huo. Kushoto ni Mwenyekiti wa mkoa wa klabu hiyo, Kadama Malunde. **PICHA: MARCO MADUHU .**

# Mbowe: Wabunge wakaidi watavuna wanachopanda

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amesema agizo la kuwataka wabunge wa chama hicho kujiweka karantini kwa siku 14, halikuwa uamuzi wake binafsi bali wa chama.

Mbowe alitoa kauli hiyo jana, akieleza kuwa wabunge waliokaidi agizo hilo, watavuna walichokipanda.

Alisema chama hakiwezi kumzuia yeyote kukihama na kina matarajio ya kupata wabunge wengi wapya katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Lazima utambue kwamba kila kwenye mzunguko wa uchaguzi, uchaguzi wa ndani ya chama au wa kiserikali kwa maana ya uchaguzi mkuu, wanatoka watu na wanaingia wengine wapya. Kila mtu atavuna alichokipanda," alionya.

Kauli hii ya Mbowe imekuja siku moja baada ya Mbunge wa Momba na Katibu wa Wabunge wa Chadema, David Silinde, kutangaza kujiuzulu nafasi yake hiyo na nyingine ndani ya chama baada ya wabunge wa chama hicho kumtaka ajiuzulu kwa kukaidi maelekezo ya kujiweka karantini.

Mbunge huyo alisema juzi kuwa alijivua nafasi ya ukatibu wa wabunge na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mbali na Silinde wabunge wengine wa Chadema waliokaidi agizo hilo ni pamoja na Mbunge wa Moshi Mjini, Jafari Michael, Mbunge wa Viti Maalum, Mariam Msabaha, Mbunge wa Kilombero, Peter Lijualikali, na Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini, ambaye tayari ameshaweka wazi atakihama baada ya kufungwa kwa Bunge la 11.

Juzi, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alinukuliwa akisema uamuzi wa kuwazuia wabunge wa Chadema kuingia bungeni kushiriki shughuli za Bunge ni wa kibabe na uongozi wa Bunge haujapendezwa na hatua hiyo.

"Wabunge ni timu moja, huwezi kwenda katika timu unatoa tu wachezaji wako, 'tokeni', hata hujajadiliana na wenzako, hamjazungumza, na hii ndiyo 'dictatorship' (ubabe) inayozungumzwa katika chama cha Chadema," Spika Ndugai alilalamika.

Hata hivyo, Spika Ndugai alisema maelekezo hayo kwa wabunge wa Chadema hayana athari yoyote kwa Bunge kuendelea kwa kuwa idadi ya wabunge wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni wengi kuliko wale wa upinzani na hivyo akidi kutimia kwa Bunge kuendelea.

**KAULI YA SILINDE**

Juzi, Silinde alisema agizo lililotolewa kwa wabunge wa Chadema kujiweka karantini kwa siku 14 lilitolewa kama tahadhari na siyo lazima.

Silinde alisema wakati huu taifa likichukua hatua za kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona, hakuona ulazima wowote wa kutoka bungeni na hakuna manufaa yoyote ambayo yangetokana na uamuzi huo.

Mbunge huyo alisema hatua ya kutohudhuria vikao halali vya Bunge vitawakosesha wananchi haki yao ya kuwakilishwa katika mojawapo ya chombo hicho kikuu cha uamuzi na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Niliamua kuendelea kuhudhuria vikao vya Bunge kwa kuwa agizo la mwenyekiti halikuwa la lazima, bali mimi nalichukulia kama ilikuwa tahadhari kwa kuwa historia inaonyesha maambukizo hayo yamepatikana maeneo tofauti na bungeni," alisema.

Silinde alisema kabla ya Mbowe kutoa agizo hilo wiki iliyopita, hakukuwa na mawasiliano wala makubaliano ya pamoja miongoni mwa wabunge wa chama hicho kuhusu uamuzi huo na aliamini ulipaswa kupata kwanza uungwaji mkono na wengi.

Katika hatua nyingine alisema kwa sasa hakuna mgawanyiko katika chama hicho ingawa baadhi ya wakosoaji ndani na nje ya chama hicho wanadhani kutokubaliana na mawazo ya mwenyekiti ni usaliti na utovu wa nidhamu badala ya kuonekana kama haki ya uhuru wa kutoa maoni.

"Kuna baadhi ya wakosoaji wa hatua hii ambayo baadhi yetu tumechukua ya kuendelea kuhudhuria vikao vya Bunge kutoka ndani na nje ya chama wakidai sisi ni wasaliti au watovu wa nidhamu, lakini ni utaratibu wa kawaida wa uhuru wa kutoa maoni bila kuathiri kanuni za chama," alisema.

Alisema kwa sasa ataendelea kuhudumia wananchi wake akiwa mwakilishi mbunge kupitia Chadema na iwapo kutakuwa na ulazima wa kuhamia kwingineko, atawasiliana na wapigakura wake ambao wataamua hatima yake kisiasa wakati wa uchaguzi mkuu ujao.

"Mimi sijanunuliwa kama baadhi ya watu wanavyodai na kwa sasa bado mbunge kupitia Chadema, iwapo kutakuwa na ulazima wa kuhama, nitafanya uamuzi kutegemea mawazo ya wapigakura wa Momba hususan wakati wa uchaguzi mkuu ujao na siyo vinginevyo," alisema.

# Mbaroni madai kumuua mama mzazi kwa panga

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

POLISI mkoani Tanga, inamshikilia Abdrahman Dihela (40), mkazi wa kijiji cha Kwachaga, Wilaya ya Handeni kwa tuhuma za kumuua mama yake mzazi kwa kumkata panga na kumtenganisha shingo na kiwiliwili kwa tuhuma za kishirikina.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Blasius Chatanda, alisema kuwa tukio hilo limetokea Mei 4, mwaka huu katika Kijiji cha Kwachaga, Wilaya ya Handeni.

Mtuhumiwa huyuo anadaiwa kumuua mama yake mzazi Asha Mwandenye (66).

Chatanda alieleza kwamba mtuhumiwa alikuwa akimtuhumu mama yake kuwa anamfanyia ushirikina na kusababisha maisha yake kuwa mabaya na kutoweza kuendelea kwa kila anachokifanya.

"Kitendo hiki ni cha kikatili sana na kwa akili za kawaida mtu huwezi kukifanya labda uwe na upungufu wa akili, tulichokifanya ni kumchukua mtuhumiwa na muda wowote kuanzia sasa atapelekwa mahakamani kusomewa shtaka lake," alisema Chatanda.

Wakati huo huo, katika kijiji cha Moa wilayani Mkinga jeshi hilo limemkamata Mohamedi Mambo (43), mkazi wa Kisosora mjini Tanga, akiwa na dawa za kulevya aina ya mirungi.

Kamanda Chatanda alieleza kwamba mtuhumiwa alikuwa akisafirisha mirungi hiyo iliyokadiriwa kuwa na kilo 250, kwa kutumia boti ndogo aliyokuwa akiendesha huku akiwa na wenzake wawili ambao walifanikiwa kutumbukia kwenye maji na kutoroka.

Alisema kuwa jeshi hilo linamshikilia mtuhumiwa pamoja na boti yake na ikithibitika kuwa yeye ndiye muhusika wa dawa hizo, boti hiyo pia itataifishwa na serikali.

Chatanda aliendelea kuwaasa wananchi mkoani hapa kufanya kazi za halali zitakazowaingizia kipato bila usumbufu wa Jeshi la Polisi kwa kuwa operesheni hiyo itakuwa endelevu ndani ya mkoa.

"Kama nilivyosema awali hili zoezi ni endelevu la kufanya operesheni zetu kila siku na kuwakamata wale wote wanaokwenda kinyume na matakwa ya serikali, wanaodhani biashara kama hizi zinafaa mimi nawakatalia na sasa watafute kazi au biashara nyingine za kufanya kwa kuwa biashara haramu itawaletea umaskini," alisisitiza kamanda.

# Hasunga alalama ma-DED kumpora mabwana shamba

## Imegeuka zama wakulima kujihudumia
## Aandaa makombora 8 kilimo kiwe 'supa'

**Na Sanula Athanas,**
ALIYEKUWA DODOMA

AWAMU iliyopita ya simulizi za mustakabali wa kilimo nchini, iligonga kwenye hatima ya korosho na 'upigaji' ndani ya Ushirika. Leo, Waziri Japhet Hasunga anafafanua namna anavyoangushwa na maofisa ugani kubadilishiwa majukumu kinyemela na mahesabu yake mapya kukirejesha kilimo kuwa ngangari. Endelea kufuatilia udadisi wa Nipashe iliyopata fursa ya faragha naye:

**SWALI: Ipo hoja kwamba maofisa tija yao imeshuka kutokana na kuwa watendaji wa kukaa ofisini. Kuna ukweli gani katika hili?**

**HASUNGA:** Kilimo chochote ili kifanikiwe kinahitaji wataalamu, na wataalamu hao ndiyo tunawaita maofisa ugani ambao ndiyo tunawategemea.

Kwenye kilimo cha mkakati, mazao ya chakula, japo siku hizi haya yote tunayaunganisha kwa pamoja, mazao ya mbogamboga na matunda, tunahitaji wataalamu ili tupande kwa utaalamu, lakini lazima tuwe na mbegu ambazo zinaweza kustahimili magonjwa, zinazoweza kuhimili ukame, na kikubwa tuwe na kilimo cha tija.

Sasa, ili kulima kwa tija na utaalamu, tunahitaji wataalamu hawa wawapo kila mahali, na ndiyo maana serikali imeamua tuwe nao. Kwa hivi sasa tunao maofisa ugani 7,330, lakini ukilinganisha na idadi ya vijiji tulivyonavyo, hao ni wachache sana, hawatoshelezi maana tuna zaidi ya vijiji 12,000.

Kwanini wamekata tamaa? Wamekata tamaa kwa sababu kwanza; hili limekuwa tatizo la msingi ambalo hata sisi wizara tunaliangalia; wale maofisa ugani wote wako chini ya Tamisemi (Ofisi ya Rais - Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa), wako kwenye halmashauri huko, manispaa na halmashauri za majiji, ndiko wanakofanyia kazi.

Kwa bahati mbaya sana, halmashauri nyingi zimekuwa zikitegemea mapato yao kwa asilimia 70 kwenye ushuru wa mazao, lakini ikija kwenye bajeti ya kuhudumia hicho kilimo, hawajaweza kutekeleza maagizo ya serikali.

Tulikuwa tumewaagiza kwamba angalau asilimia 40 ya hayo mapato yaende kwenye maendeleo kikiwamo kilimo. Kwa sababu kilimo ndiyo kinawapa mapato makubwa, watenge bajeti ya kuendeleza hicho kilimo, lakini kwa bahati mbaya halmashauri nyingi hazitengi kabisa bajeti ya kuendeleza kilimo.

Yale maeneo ya kiutendaji, utakuta kwamba wamejikita zaidi kwenye elimu, afya, barabara na miundombinu iliyo chini ya Tarura, maji na maeneo mengine, lakini kilimo ambacho kinawapa mapato, hakijapewa uzito na kwenye bajeti kinapewa fedha kidogo sana.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akiteta jambo na wakulima hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

Hili limewakatisha tamaa maofisa ugani. Utakuta hawana bajeti ya kufanyia kazi, hawana vitendeakazi, hawana usafiri na pia mara nyingine watendaji kwa maana ya wakurugenzi wa halmashauri wamekuwa wakiwahamisha. Badala ya kufanya kazi za wizara ambazo ni za kilimo, wanawaambia waende kukusanya mapato.

Kwa hiyo, wanapangiwa kazi za kiutendaji, wanakuwa watendaji wa vijiji, kata, wanakwenda kukusanya mapato. Ile kazi ya msingi ya kusimamia kilimo wamekuwa hawaifanyi. Hii imewakatisha tamaa na kuwafanya wasiwajibike ipasavyo.

Sisi kama wizara tumeona kuna haja tuone namna tunavyoweza kuwatumia na kuhakikisha tunakaa na Tamisemi ili kuongeza tija na morali kuhakikisha hao watu wanafanya kazi sawasawa.

Sasa, nini cha kufanya? La kwanza. kuna sheria ambayo ilipitishwa mwaka 2006 chini ya marekebisho madogo ya sheria, ambayo inatamka kwamba wataalamu wote walioko Tamisemi, wanapaswa kuhudumiwa na wizara za kisekta zinazohusika.

Na sisi tumeamua kuchukua hili jukumu, tukae vizuri na hao wataalamu wetu, maofisa ugani. Tuone namna gani tunaweza 'kuwa-motivate' (kuwahamasisha), tuone namna gani tunavyoweza kuwasaidia kuwapatia vitendeakazi ili wasimamie kilimo kiwe na tija.

**SWALI: Wizara ina mikakati ipi kuhakikisha mazao makuu ya biashara yanaongezwa ubora na kuwa na uhakika wa soko ndani na nje ya mipaka ya Tanzania?**

**HASUNGA:** Mazao ya kimkakati tunayo mengi kwa sasa na yanasimamiwa na bodi za mazao. Lakini, pamoja na mazao haya kuingiza fedha nyingi za kigeni, bado tulikuwa hatujawa na mkakati wa kuongeza uzalishaji.

> "Kwa bahati mbaya sana, halmashauri nyingi zimekuwa zikitegemea mapato yao kwa asilimia 70 kwenye ushuru wa mazao, lakini ikija kwenye bajeti ya kuhudumia hicho kilimo, hawajaweza kutekeleza maagizo ya serikali

Hivi sasa tuna mkakati kwanza wa kuongeza uzalishaji. Mfano, kahawa tuna mpango kuongeza uzalishaji, pamba tuongeze uzalishaji na korosho vilevile.

Korosho tunataka tutoke sasa hivi kwenye uzalishaji wa tani 225,000 hadi tani 600,000 kwa msimu na lengo letu kubwa ni kufika tani milioni moja. Hili linawezekana kwa mkakati mkubwa ambao tumeupanga wa kuongeza mikoa ya uzalishaji. Imeongezeka kutoka mikoa mitano hadi 20.

La pili ni kuhakikisha tunakuwa na mkakati wa kuhakikisha tunafanya utafiti wa mbegu bora zenye uwezo wa kuongeza uzalishaji na la tatu kuongeza zaidi utaalamu na mambo mengine.

Jambo lingine ambalo tunataka kulifanya ni kuongeza thamani. Tumefikiri kwamba kwa sasa Tanzania badala ya kuuza mazao yakiwa malighafi, lazima tuyaongezee thamani kidogo. Ili mkakati huu ufanikiwe, ni lazima kujenga viwanda.

Mfano, chukulia kahawa, huwezi kuiuza kama ilivyo, inabidi 'ui-process' hadi kiwango fulani, eeeh, chai lazima 'ui-process' mpaka 'level' fulani. Vivyo hivyo, korosho lazima ibanguliwe ifikie hadi kiwango fulani.

Tunataka pia mazao kama mkonge, pamba nayo yatumike kwanza humu ndani kwenye viwanda vyetu vya katika kuyaongeza thamani, tufikie kwenye kiwango cha kutengeneza nyuzi, tuuze majola.

Tunataka mazao yote ya kimkakati pamoja na yale mawili tuliyoongeza -- tumeongeza mchikichi, tumeongeza alizeti ili kujitosheleza kwa mafuta ya kula baada ya muda mrefu kuwa tunaagiza nje ya nchi, yanatusaidia kuanzisha viwanda nchini.

Jambo lingine la msingi ni kuhamasisha wawekezaji kuja kujenga viwanda. Utaona kwenye korosho tumefanya hivyo, kwenye kahawa tumefanya hivyo, lakini kwenye mkonge tunataka tufanye hivyo na kwenye pamba tunahakikisha vinakuwapo viwanda vya kutengeneza nguo, vya kutengeneza nyuzi.

Tunataka tufanye hivyo ili tuondokane na dosari ya kuuza mazao yetu yakiwa malighafi. Ukiuza yakiwa malighafi, maana yake utakuwa unatengeneza ajira nje ya nchi, utauza kwa bei ndogo. Ninasema hili litatusaidia.

Lakini pia kuna jambo lingine ambalo tunataka tulifanye -- kutafuta masoko ya uhakika. Tunataka tuingie mikataba na baadhi ya kampuni, na baadhi ya nchi.

Tuuwe na mikataba ya kudumu ili kwamba tunauziana, tunataka tuwauzie kitu hiki, tuwe tunakubaliana bei, tunatumia mikataba kama inavyofanyika kwenye biashara za kimataifa.

Na hili msimamo wetu ni kuongeza kilimo cha pili, kilimo cha mkataba. Kwa mfano, kwenye tumbaku tumefanya hivyo, tuna kilimo cha mkataba. Tunataka tuongeze hicho kitu ili mazao mengi yawe na kilimo cha mkataba.

Katika kilimo cha mkataba, unakuwa na uhakika soko lipo. Ukivuna una uhakika wa kwamba utauza kwa bei fulani. Kwa hiyo, hata kama unakwenda kuwekeza, unakuwa umepiga hesabu zake vizuri zaidi. Tunataka tuwekeze ndani ya msingi wa namna hii.

Jambo la lingine tunalotaka kulifanya kwa sasa, tunataka kwenda kwenye mfumo mwingine wa kuuza mazao. Badala ya kutegemea kwamba wanunuzi waje hapa, hasa katika kipindi hiki ambacho kuna mlipuko wa corona, hawatakuja kwa sababu wamekuwa 'locked down'.

Tunategemea zaidi kuanza kutumia mtindo ule wa kutumia TMX, soko la bidhaa ambalo litakuwa linauza kwa mitandao. Kwa hiyo, tunatangaza dunia nzima kwamba Tanzania itauza korosho tani kadhaa za 'grade one' (daraja la kwanza), tani kadhaa za 'grade' kadhaa, au tunaendesha mnada kwa kutumia huo mtandao, anayeshinda ndiyo mnakuja kutia saini mkataba wa 'delivery', basi mnakuwa mmekwenda vizuri.

Tunaamini hiyo itakuwa inatusaidia kupata masoko mazuri, lakini kuondokana na hii dosari ambayo imejitokeza kwa kipindi hiki na itawafanya wananchi wawe na uhakika wa masoko ya moja kwa moja.

La mwisho, tunataka kabisa tuhakikishe kwamba kwa sasa tunaingia kwenye mikataba ya moja kwa moja, yaani 'direct selling'. Hii selling tulikuwa hatujaingia nayo mikataba sana.

Tunataka 'tu-promote' (kukuza) ile ili wakulima wanaingia mkataba moja kwa moja labda na wanunuzi wa Ulaya, Marekani au Australia, New Zealand kwa kusainishana mikataba kwamba sisi ukituletea muhogo, tunahitaji tani kadhaa zenye muhogo wa kiwango hiki, yaani muhogo uwe wa kiwango fulani.

Basi tutasainishana hiyo mikataba, ninyi kazi yenu inakuwa kuzalisha tu na kuhakikisha kwamba mnapeleka sehemu ambayo mlikuwa mmekubaliana.

Hii itasaidia sana kuhakikisha masoko ya uhakika yanapatikana. Lakini tutaweza kujenga viwanda, wawekezaji wakawa na viwanda vya kuongeza thamani.

- **KESHO PATA SIMULIZI ZA WAZIRI HASUNGA KUHUSU VIZINGITI SABA VINAVYOMDONDOSHA MKULIMA WA KITANZANIA ASIINUKE.**

# Katibu Tawala msaidizi mkoa, wengine wawili wafariki ajalini

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WATU watatu akiwamo Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Singida, wamefariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria, aina ya Toyota Landcruser Hardtop, mali ya idara ya afya ya mkoa wa Singida, kugongana uso kwa uso na basi la abiria.

Basi hilo ni mali ya kampuni ya Happy Nation eneo la Magole wilayani Kilosa, Barabara Kuu ya Morogoro-Dodoma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo juzi usiku huko maeneo ya Feri, Tarafa ya Magole.

Alisema ajali hiyo imehusisha basi la abiria aina ya Higer yenye namba za usajili T 483 DRF kampuni ya Happy Nation lililokuwa likitokea Mwanza kuelekea Dar es Salaam, ikiendeshwa na Isack John, mkazi wa Dar es Salaam.

Aliwataja waliofariki dunia ni Guhacha Kitinda (60), mkazi wa Singida ambaye kwa mujibu wa taarifa kutoka Singida, ni Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa huo.

Wengine ni Sabinaeva Guhacha, mkazi wa Singida na Baptist Beda (37), ambaye alikuwa dereva wa gari dogo.

Mutafungwa alisema katika ajali hiyo mtu mmoja, Michael Matonya (20), mkazi wa Kibaigwa aliyekuwa abiria wa pikipiki alijeruhiwa katika ajali hiyo, na amelazwa Hospitali ya Mtakatifu Joseph Dumila wilayani Kilosa.

Alitaja chanzo cha ajali hiyo kuwa ni dereva wa basi kujaribu kuipita pikipiki iliyokuwa mbele yake bila kuchukua tahadhari, hivyo kukutana uso kwa uso na gari dogo.

Miili imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, na dereva wa basi alitoroka baada ya ajali.

# Wabunge wataka jeshi lisitumike uchaguzi mkuu

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wamelitaka Jeshi kutokubali kutumika wakati wa Uchaguzi Mkuu, kutoa fedha za utafiti wa corona, kuongeza mishahara ya Suma JKT na ulipaji wa fidia wananchi waliochukulia maeneo yao.

Wabunge hao alitoa maoni yao wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka huu wa fedha, na hotuba kuwasilisha bungeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jennista Mhagama.

Mbunge wa Mtambile (Cuf), Masood Abdallah Salim, alisema kuwapo kwa magari hayo ni kuruhusu kutumika kutisha wananchi kwenye uchaguzi huku akihoji kama ni uchaguzi wa kiraia kwa nini magari ya jeshi yapite.

"Hakuna vita magari yasipitishwe mtaani, waacheni wananchi wachague, msiruhusu kuacha magari ya jeshi kutembea siku tano au wiki moja kabla ya uchaguzi," alisisitiza.

Kuhusu janga la corona, Mbunge huyo alitaka wizara hiyo kutoa taarifa za wapendwa wao ambao wako nchi mbalimbali kwa ajili ya kulinda amani.

"Tunajua corona imesambaa duniani na tuna askari wetu wako maeneo mbalimbali kulinda amani, ni vyema tukajua hali zao kwa sasa zikoje," alisema.

Pia, alitaka wizara kutoa fedha za kulipa fidia wananchi kwenye maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi, kwa kuwa kumekuwa na ucheleweshaji kiasi cha wengine kufariki.

Alisema Suma JKT kwenye kitengo cha ujenzi na kwamba ni vyema ubora wa kazi zao wamejenga nyumba ngapi na ubora wake, ijulikane ni fedha kiasi gani imepatikana.

Kadhalika, alisema Suma JKT ambao wanalinda ni vyema idadi ikajulikana, huku kukiwa na malalamiko ya mishahara yao ambayo ni Sh. 190,000 kwa mwezi ambayo ni ndogo kwao.

"Ninaomba waongezewe kiasi hiki ni kidogo sana, wanalalamika wanapokuwa kwenye sehemu za ulinzi," alisema.

Naye, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Mariam Msabaha, aliiomba serikali kuwaangalia na kuwawezesha vizuri wanajeshi katika kipindi cha uchaguzi mkuu kwa kuwa wanalinda mipaka na huenda kukawa na wachokozi.

Aliiomba serikali kuwakopesha fedha ili wajenge nyumba uraiani kwa kuwa siyo vizuri wanapostaafu kwenda kuhangaika na maisha. Naye, Mbunge wa Jimbo la Kijitoupele (CCM), Shamsi Vuai Nahodha, alisema jeshi lipewa fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya utafiti wa maradhi ya binadamu ikiwamo corona na kwamba uzoefu unaonyesha kuwa nchi kubwa zinatumia majeshi kufanya utafiti.

Pia, alitaka lifanye utafiti wa 'Micro-biology' kwa kuwa mjadala na malumbano unaendelea kati ya mataifa makubwa ni kwamba kuna jambo la kimaabara limefanya kuhusu chanzo cha maradhi ya corona.

"Mtakumbuka siku za nyuma mataifa makubwa yalitumia silaha kali kuangamiza, haitashangaza kama atatumia biolojia kuangamiza watu, ndiyo maana ni vyema jeshi likafanya utafiti,"alisema Nahodha ambaye amewahi kuwa Waziri Kiongozi wa Awamu ya Sita wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.



Mkazi wa Kitwiru Mjini Iringa na askari polisi wakitazama kaburi (kulia), ambalo baada ya kulifukua halikuwa na maiti, lililokutwa juzi jioni katika kiwanja cha askari wa kikosi cha usalama barabarani mkoani humo, huku wahusika wa tukio hilo, wakiwa hawajajulikana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Taharuki wananchi kukuta kaburi kiwanja cha askari

**Na Francis Godwin,** IRINGA

TAHARUKI imeibuka kwa wananchi wa Kitwiru Manispaa ya Iringa, baada ya kukuta kaburi jipya kwenye kiwanja walichodai ni cha askari wa usalama barabarani na kulazimika kuweka ulinzi wakisubiri lifukuliwe.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12 jioni baada ya wananchi wa eneo hilo kubaini uwapo wa kaburi hilo katika makazi ya watu ambalo lilikuwa limefukiwa siku mbili zilizopita.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi wa eneo hilo waliokuwa wakishuhudia ufukuaji wa kaburi hilo chini ya usimamizi wa polisi, walisema eneo hilo ni la makazi ya watu na wameshangazwa kuona kaburi bila kujua nani wamefanya mazishi hayo.

Mkazi wa eneo hilo John Sanga, alisema kiwanja kilichokutwa kaburi kiliuzwa kwa askari mmoja na sababu za watu kufanya tukio hilo hazijafahamika.

Rose Ng'umbi, mkazi wa Nyamhanga B, ambaye ndiye mmiliki wa awali wa kiwanja hicho, alisema waliuza kiwanja hicho na hakuna mgogoro wowote wa eneo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyamhanga, Nasson Lusasi, alisema wamelazimika kuita polisi baada ya wananchi zaidi ya 1,000 kukusanyika katika eneo hilo toka juzi jioni kutaka kufukua kaburi hilo.

Alisema polisi walilifukua kaburi hilo lililokuwa na urefu wa mita mbili na kukuta chupa na jiwe.

Alisema tukio hilo linawachanganya kwa kuwa siku za hivi karibuni kumekuwapo na matukio ya watu kuuawa, na polisi wamefanikiwa kudhibiti.

Askari anayemiliki kiwanja hicho, Fatma Mkwawa, alisema alipigiwa simu kuelezwa kuhusu kaburi hilo katika kiwanja chake na kueleza kuwa waliofanya hivyo walikuwa wakijaribu kumtisha.

Diwani wa Kata ya Kitwiru, Baraka Kimata, alisema sababu ya wananchi kuweka ulinzi katika kaburi hilo ni kutaka kujua kilichozikwa ndani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alisema baada ya kufukua hawajakuta kitu na kuwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa polisi wanapokuwa na mashaka na jambo ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyama vya ushirika vilivyobaki vijitathmini

**SERIKALI** imevifuta vyama vya ushirika 3,348 ambavyo vilikuwa havifanyi kazi, ama kutotekeleza majukumu yake ya msingi na vyama hewa.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitoa tangazo hilo juzi jijini Dodoma, na kueleza uamuzi huo unatokana na kusudio la serikali alilotangaza Januri 5, mwaka huu, la kutaka kuvifuta vyama hivyo.

Akisema kwa mujibu wa kifungu cha 100 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6, ya mwaka 2013 na kanuni ya 26 ya kanuni za vyama vya ushirika za mwaka 2015, serikali ilitoa notisi ya siku 90 ya kusudio la kuvifuta vyama 3,436 kutoka katika daftari (Rejista) la vyama vya ushirika.

Alisema katika notisi hiyo, serikali ilitoa nafasi kwa mtu, chama au taasisi yoyote yenye mapingamizi kuhusu kufutwa kwa vyama hivyo vya ushirika vilivyoorodheshwa kuwasilisha kupitia ofisi za warajis wasaidizi wa mikoa.

Alifafanua kuwa notisi hiyo iliisha Aprili 17, mwaka huu na hivyo kumwezesha kuvifuta vyama ambavyo havijajitokeza kupinga.

Aliongeza kuwa kabla ya muda wa kutoa mapingamizi kumalizika, serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ilipokea jumla ya mapingamizi 88, ambayo yalichambuliwa na kufikiwa uamuzi wake kwa kuzingatia maoni ya Warajis wasaidizi wa mikoa husika.

Alisema kutokana na hali hiyo, serikali imejiridhisha na kukubaliana na mapingamizi hayo ya kutofutwa kwa vyama 88, na kuwa Warajis wasaidizi wa mikoa watawajibika kusimamia vyama hivyo vinavyoendeshwa kwa matakwa ya sheria.

Ili kuendeleza na kuurejesha katika mstari ushirika, ambao katika miaka ya karibuni ulizorota kutokana na vitendo vya wizi, ubadhirifu, uzembe, usimamizi mbovu na kutokuwajibika kwa viongozi, tunaona kuwa serikali imefanya uamuzi mzuri.

Sote ni mashahidi kuwa, kuna watu wengi ambao wameanzisha na kuendesha vyama vya ushirika vikiwamo vya kuweka na kukopa Saccos hewa kwa lengo la kujinufaisha kupitia wizi na vitendo vingine vinavyofanana na hivyo.

Kama serikali ilitoa notisi kuhusu nia ya kuvifuta vyama hivyo, ili kuvipa fursa ya kuwasilisha pingamizi ndani ya siku 90, na 88 kukubaliwa sababu za kutofutwa , basi serikali haikuwa na lingine la kufanya zaidi ya kuvifutia usajili.

Vyama vilivyofutwa na idadi kwenye mabano ni Saccos (2,513), Amcos (229), mifugo (77), vyama vya walaji (27), vyama vya huduma (70), vyama vya ufugaji nyuki (15), nyumba (9), madini (22), viwanda (79), uvuvi (32), umwagiliaji (31) na vinginevyo (244).

Vyama vilivyobaki baada ya kufutwa kwa vyama 3,348, kwa sasa Rejista ya vyama vya ushirika nchini itabaki na jumla ya vyama 8,611.

Tunaelewa kuwa uamuzi huo utakuwa umewaumiza baadhi ya wanaushirika wasio na hatia, lakini serikali haikuwa na jinsi ya kukwepa kutekeleza wajibu wake wa kusimamia sheria za nchi.

Pia serikali ilipata ushauri kutoka kwa warajisi wasaidizi wa mikoa na wilaya, ambao wanavijua vizuri vyama hivyo kutokana na kuwa katika maeneo yao.


Ushauri wetu kwa vyama vya ushirika 8,611 vilivyobakia ni kuheshimu na kufuata sheria ikiwamo kufavya kazi za ushirika, hivyo kurejesha hueshima ya ushirika ambayo vilijijengea kwa miaka mingi.

Vyama hivyo havinabudi kujitathmini upya kuhusiana na nini vikifanye katika kutoa huduma za ushirika kwa wanachama wao kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Hatutarajii kuona au kusikia kuna chama cha ushirika hewa au cha mfukoni.

Tunaishauri serikali uhakikishe inafuatilia shughuli za ushirika nchini ili vyama vikidhi malengo yake ya kutoa huduma kwa wanachama wake. Katika kufanikisha hilo, utaratibu wa serikali kuvifuta vyama vitakavyokwenda kinyume cha sheria hauna budi kuwa endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

# Enyi Mabibo sokoni, hii nini kuoshana miguu na corona?

**SERIKALI** imeendelea kuhamasisha vita dhidi ya maradhi ya corona. Namna inavyopiganwa ni kwa kujituma kunawa mikono kila mara, kuzingatia tahadhari, kupitia busara ya kutoshiriki mikusanyiko isiyo ya lazima.

Pia, katika kupiga chafya, kuna matumizi ya mfumo unaomlinda mwenzako, kwani kanuni nzuri za kiafya zinahimizwa kila mara watu wazitumie kama vile kujikinga kwa kiwiko.

Hapo nikiri kwa kiasi kikubwa jamii imekiri kwa kuitikia wito ni jambo jema, hata katika mtazamo wa kiimani. Kwa sasa maduka na hata nyumba za watu zimekuwa na ndoo za maji ikiwamo na sabuni, watu wananawa kabal ya kuingia.

Nianze kupazungumzia soko la Mabibo, jijini Dar Salaam lililopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Kutokana na kuwapo ugonjwa wa corona, mamlaka husika ilizuia biashara ya kunawisha watu katika mlango mkuu wakiingia watu na kutoka.

Kimsingi, soko la Mabibo ni maarufu kwa ajili ya vyakula mbalimbali, vinavyoingizwa jijini Dar es Salama, likiwa na sifa ya kipekee ya biashara ya kuuzwa ndizi za kupikwa. Eneo hilo la mlangoni linajulikana sana, kwa hali isiyo bora kiafya na tope jingi.

Ni miaka mingi sasa kumekuwapo biashara, hasa watu wanapoingia na kutoka, unawishaji unaofanyika kwa bei ya shilingi 200, maana uchafu huo haukwepeki.

Lakini kama inavyojulikana, kutua kwa corona kumeleta yake kila upande. Maagizo na mabadiliko mengi yakienda na marufuku. Sokoni Mabibo ni sehemu ya walioagizwa kuwapo shida.

Pamoja na kuondolewa sokoni, wasifanye biashara hiyo, wanaoshaji miguu sokoni Mabibo, bado wapo wanaendelea kutoa huduma hiyo, katika mazingira ya kujificha.

Tukiangukia elimu inatutaka tujikinge, lakini sisi wananchi tunakuwa wakaidi wa maagizo tunayopewa, wakati kufanya hivyo ni hatari kubwa na mtu ana uwezo wa kupata maambukizi ya maradhi corona.

Pia, kilicho kibaya zaidi ni waoshaji hao hawana vifaa vya kuvaa kukinga mikono yao wanapokuwa wanatoa huduma hiyo kunawisha watu miguu.

Kupitia soko hilohilo, pamoja na kuwekwa maji na sabuni, bado kunashuhudiwa baadhi ya wabeba mizigo hawanawi mikono yao wanapokuwa wanakimbizana na mizigo yao, ambayo mingi ni mikubwa na hasa magunia yaliyosheheni.

Hata askari waliopo hapo mlangoni wanaojitahidi kuwaita wabeba mizigo wanawe mikono, wapo ni baadhi ya watu waelewa, lakini kuna kundi la wasio na uelewa wanakataa kunawa mikono yao ya kila siku.

Na hili wanajamii walioko sokoni Mabibo walielewe hili, kwamba hatua hiyo haiwahusu peke yao, kwani katika masoko mengine mengi nchini hilo linafanyika na daima hakuna la ukaidi unaoendelezwa katika eneo hilo.

Hata tukijisogeza katika vituo vuya mabasi, tunashuhudia ndoo na sabuni na hasa katika vituo vya mwisho makondakta na madereva wameelimika vilivyo katika hilo, wakiwelekeza abiria wao kutumia. Sasa inakuwaje ndugu zetu wa Mabibo Sokoni kukaidi?

Tunapotamka serikali, ina maana ni sisi watu, mimi na wewe na si lingine. Maana yake, kutekeleza ya serikali ni mimi na wewe kuwa katika mkondo mnyoofu unaoeleweka.

HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Shirika la Holt Dream Center la Korea Kusini, Park Jieun (kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali vikiwamo unga na vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa corona kwa Janeth Mwanjela, mmoja kati wenye kaya masikini 109 za Keko Mwanga 'B', jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wise, Dk. Astronaut Bagile. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Ndugai aagiza wabunge wa Chadema warejeshe posho

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

SPIKA Job Ndugai ametangaza uamuzi mgumu dhidi ya wabunge wa Chadema walioamua kutohudhuria vikao vya Bunge kutokana na tisho la virusi vya corona.

Amewataka kurejesha zaidi ya Sh. milioni 110 walizolipwa kwa wiki mbili ili kuhudhuria vikao vya Bunge na iwapo hawatafanya hivyo, watakamatwa na vyombo vya dola.

Spika Ndugai alitangaza uamuzi huo jana, akisema alishangazwa na kusikitishwa na agizo la Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, kuwalekeza wasihudhurie vikao kwa wiki mbili.

"Nimeshangazwa sana na tangazo lile na nimesikitishwa sana kwa sababu hana mamlaka ya kuitisha utoro na mgomo kwa wabunge," alisema.

Spika Ndugai alisema taarifa alizonazo wabunge hao wanazurura na kwamba barua ya Mbowe siyo halali na hawataitambua na haina nafasi kwa Bunge hilo.

"Wabunge hao (Chadema) kokote waliko warudi haraka kuendelea na kazi zao, watakaondelea na mgomo wajue baada ya wiki mbili hawatapokewa bungeni, isipokuwa kama watapima corona na kupata vyeti rasmi kabla ya kukanyaga geti la Bunge na hayo ndiyo maelekezo," alionya.

Kwa mujibu wa Spika, wabunge hao wakati wanaondoka walishalipwa fedha za kujikimu kuanzia Mei Mosi hadi 17, jumla ya Sh. milioni 110.16 na kwamba wakiendelea na vikao hawatadaiwa.

"Ninaagiza wabunge hao, kuanzia Mbowe kurudisha Sh. milioni 2.04 alizolipwa, wenzake wote kurudisha Sh. mil 2.04 walizolipwa kila mmoja kwa vile ni utoro wa hiari kwa maneno rahisi ni wizi," alisema.

Spika Ndugai aliwataja Catherine Ruge, Devotha Minja na Joyce Mukiya, Roda Kunchela, Zainabu Mussa Bakari na Zubeda Hassan Sakuru waliolipwa Sh. milioni tatu kila mmoja.

"Maagizo yangu ni nini? Hawa kila mmoja wao arudishe hizi fedha, atakayefika getini anapohesabu mgomo wake (siku 14 za kujitenga) hataingia katika eneo hili na hataweza kupokewa.

"Na baada ya wiki mbili kwisha kama hawatarudisha fedha hizo, nitapeleka orodha hiyo kwenye vyombo vya ulinzi na usalama na Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatusaidia kuona tunakwenda vipi.

"Wao si wababe bwana na wapo mwisho mwisho (kumaliza Bunge), wajue wanacheza na moto, yanayofuata yanafurahisha zaidi," alisema.

Spika pia aliisoma barua ya Katibu wa Chadema, John Mnyika, iliyotaka Bunge kutomtambua Cecili Mwambe kama Mbunge wa Ndanda na kumlipa stahiki zake.

"Barua yenyewe ni fupi, ngoja niwasomee, anasema Cecil Mwambe, alikuwa Mbunge wa Jimbo la Ndanda, aliyedhaminiwa na Chadema na Februari mwaka huu alitangaza kupitia vyombo vya habari amehama chama.

"Kwa mujibu wa ibara ya 7(f) ya Katiba amekoma kuwa mbunge na ameacha kiti chake katika Bunge, kwa hiyo Bunge lisiendelee kumpatia stahiki zozote."

Spika alisema anamshangaa Mnyika kwa kuwa maneno anayosema alipaswa aambatanishe na barua ya Mwambe inayothibitisha anayosema Mnyika na hajafanya hivyo.

"Pili, sina barua ya Mwambe kusema kaacha ubunge kwa hiari yake mwenyewe, na kama ni chama hiki kimechukua hatua sina viambatanisho vinavyoonyesha vikao halali vilivyofanya maamuzi haya. Kwa hiyo, hii barua haina maana, haina mantiki.

"Nawaambia wabunge wote ikiwamo wa Chadema mnaotishwatishwa huko kuwa mnaye Spika imara, atawalinda mwanzo mwisho. Habari ya ukandamizaji na ubabaishaji hauna nafasi, fanyeni kazi zenu kwa kujiamini, mmeaminiwa na wananchi," alisisitiza.

Spika Ndugai pia alilijulisha Bunge kuwa mahakama imetupilia mbali maombi ya Tundu Lissu kuhusu ubunge wake na kumtaka kujiandaa kulipa gharama za kesi.

## Waliopisha maeneo ya jeshi kulipwa fidia bil. 8/-

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imesema itatumia zaidi ya Sh. bilioni 8.18 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya shughuli za jeshi.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema wanahakikisha fedha hizo zinawafikia wahusika.

Alisema pia Sh. bil. 2.11 zitatolewa kwa malipo ya hati za madai ya makandarasi kwenye miradi ya jeshi.

Alitolea mfano wa eneo la Ilemela kwa Mei walileta madai ya Sh. bilioni 6.195 na baada ya uhakiki zilibainika ni Sh. bilioni 6.165, na kwamba hadi Juni 30, mwaka huu watakuwa wamemaliza kulipa.

"Tunatoa kipaumblea cha juu sana kwamba maeneo yanayotolewa na jeshi wananchi wanalipwa kwa wakati," alisema Waziri Mpango.

Kuhusu wastaafu, alisema serikali inatambua mchango wao na anahakikisha anapata stahili zao na pensheni ili alitumikie taifa vizuri.

Naye, Waziri wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jennista Mhagama, akijibu hoja za wabunge, alisema kwa mwaka 2020/21 imetegwa Sh. bilioni 21 kwa ajili ya kulipa fidia.

Mhagama aliwasilisha bajeti kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Waziri huyo alitoa ufafanuzi huo, kutokana na wabunge kulalamikia kuchelewa kwa malipo ya fidia kwa wananchi pamoja na malipo kwa wastaafu.

# Serikali yaona shida mpaka wa Msumbiji

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), imeeleza changamoto iliyopo kwenye baadhi ya mipaka, ikiwamo kuwapo kwa kikundi cha kigaidi kinachoshambulia Jimbo la Cabo Delgado nchini Msumbiji linalopakana na mkoa wa Mtwara.

Hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2020/21, iliwasilishwa bungeni jana kwa niaba ya Waziri husika, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jennista Mhagama.

"Hali ya ulinzi na usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, usalama wa mpaka huu unatishiwa na kundi la kigaidi la Ansar Al Sunnah Wa Jamaah (AASWJ) katika mpaka wa Msumbiji ambalo linaendelea kufanya uhalifu nchini Msumbiji katika Jimbo la Cabo Delgado.

"Eneo lenye mgogoro lipo jirani na mpaka wa nchi yetu mkoa wa Mtwara). Katika hatua ya kuimarisha ulinzi wa mpaka huu, mwezi Machi, mwaka huu, serikali ilipeleka vikundi vya ulinzi katika maeneo ya Msimbati na Sindano, mkoa wa Mtwara na Chiwindi katika Wilaya ya Nyasa Mkoa wa Ruvuma," alifafanua.

Aidha, alisema hali ya usalama wa mpaka wa Tanzania na Malawi imeendelea kuwa shwari kwani hakuna tishio la wazi dhidi ya nchi na kwamba changamoto ya mpaka katika Ziwa Nyasa inaendelea kufanyiwa kazi.

"Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kutumia njia za kidiplomasia, ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu, na kwamba pande husika zimetakia zisijishughulishe na utafiti wa kiuchumi katika eneo lenye mgogoro," alibainisha.

Aidha, waziri huyo alibainisha changamoto zilizopo kwenye mipaka hiyo ni kuendelea kuwapo kwa migogoro na viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi ambazo Tanzania inapakana nazo,na kuwa chanzo cha wakimbizi na wahalifu kuingia nchini.

"Juhudi zinaendelea kufanyika kuhakikisha alama za kudumu za mipaka zinawekwa katika maeneo ya Taifa letu," alisema.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akizungumza, baada ya kupokea vifaa tiba kutoka kwa Mkurugenzi wa Rasiliamali Watu na Utumishi wa Benki ya Absa Tanzania, Patrick Foya (kushoto), ikiwa ni mchango wa kusaidia juhudi za serikali mapambano dhidi ya maambukuzo ya virusi vya corona. Vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 20 vilikabidhiwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wataalamu majengo kuhakiki nyumba za mafuriko Missenyi

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

WILAYA ya Missenyi mkoani Kagera, imesema itatuma wataalamu wa majengo ili kwenda kuhakiki kama nyumba za wananchi zilizojaa maji kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha, zinaweza kuendelea kutumika.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Kanali Denice Mwila, wakati akipokea msaada wa unga kilo 1,600, maharage kilo 320, vyandarua 200, mablanketi 248 na dawa za kutibu maji vidonge 120,000, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi milioni 16.7, kwa ajili ya wananchi wa vijiji vya Mabuye, Omundongo, Kasambya na Burifani, ambao nyumba zao zimejaa maji na kulazimika kutafutiwa hifadhi. Kanali Mwila alisema nyumba nyingi za wananchi zimejengwa kwa udongo na kuwa zinapojaa maji yanaondoka na udongo na kuacha matofali.

"Wananchi wengi wanapojenga nyumba wanatumia udongo badala ya saruji katikati ya tofali moja na tofali jingine, kwa hiyo nyumba zikijaa maji yana kawaida ya kuondoka na huo udongo, na zinakuwa sio salama tena," alisema.

Alisema wananchi wanaoishi katika vijiji hivyo wanapaswa kujiandaa kuhama katika maeneo hayo hatarishi, ili waweze kuwa salama.

"Tuwe wakweli maeneo haya ni njia za maji, na kawaida maji huwa hayasahau njia zake, cha muhimu ni wananchi kujiandaa kuhama ili kuepusha madhara yanayoweza kuwakumba ikiwamo uharibifu wa mali na wakati mwingine vifo," alisema.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya meneja wa World Vision Mkoa wa Kagera, mwakilishi wake, Victor Nsiima, aliwataka wananchi walioathirika kutouza misaada wanayopewa ili wasiwakatishe tamaa watu wanaojitoa kuwasaidia.

Jumla ya kaya 106 zenye watu zaidi ya 400 katika Wilaya ya Missenyi hazina mahala pa kuishi, kutokana na nyumba zao kujaa maji kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha, hali iliyosababisha wananchi wa vijiji hivyo vinne kuhamishiwa katika shule za msingi S.K. na Omundongo.

# CWT yatoa mil. 3/- za ukarabati miundombinu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimetoa msaada wa Sh. milioni tatu kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya walimu iliyoathiriwa na mafuriko Wilaya ya Kibiti na Rufiji, mkoani Pwani.

Akikabidhi msaada huo ambao utatumika kununua mifuko ya saruji 200 itakayotumika katika wilaya hizo, Mtunza Hazina wa CWT, Abubakary Alawi, alisema wameamua kuunga mkono juhudi za serikali kuweka mazingira mazuri ya kufundishia kwa walimu.

Alawi alisema, pamoja na kuwa CWT ni chama cha kutetea maslahi ya walimu, lakini kwa sasa wameamua kuungana katika kusaidia kurejesha miundombinu ya walimu ambayo imeharibiwa na mafuriko.

"Tumeguswa na hali ya taharuki iliyowapata walimu wenzetu wa Rufiji na Kibiti, tumekuja kutoa mchango wetu kwako mkuu wa mkoa," alisema.

Akipokea msaada huo Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alishukuru kwa msaada huo na kuomba kampuni zingine ambazo zimewekeza katika mkoa huo kuiga mfano wa CWT.

"CWT ni taasisi inayojitambua, inayoshughulika na matatizo ya wananchi na katika hili niwapongeze kwa kuunga mkono juhudi za serikali."

Serikali haiwezi kujenga barabara zote nichukue fursa hii kuwaomba wadau wengine na wamiliki wa viwanda Pwani kuiga na kusaidia changamoto zilizopo Kibiti na Rufiji," alisema.

Ndikilo alisema, mafuriko yaliyotokea katika wilaya hiyo na kusababisha maafa kwa wananchi yametokana na mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha mabwawa ya Mtera na Kidatu kufunguliwa na hivyo maji kufurika kwenye mashamba na makazi ya watu.

# Nditiye apokea mabehewa 20 Bandari kavu Kwala

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, ameshiriki katika mapokezi ya treni ya kwanza iliyobeba mabehewa 20 za mizigo kutoka Dar es Salaam na kuwasili Bandari kavu ya Kwala iliyopo Kibaha, mkoani Pwani.

Katika mapokezi hayo yaliyofanyika jana, viongozi mbalimbali wa serikali walishiriki akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Everist Ndikilo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari, Deusdedit Kakoko, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli, Masanja Kadogosa na wafanyakazi.

Nditiye alisema bandari hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, itasaidia utunzaji wa Barabara ya Morogoro kwa kuwa bila Bandari ya Kwala mizigo ingepaswa kusafirishwa na malori ambayo yangeharibu barabara hiyo.

Alisema kufuatia hatua hiyo hivi sasa wafanyabiashara watakuwa wanachukua mizigo yao katika bandari kavu ya Pwani.

"Niwahakikishie Watanzania na wadau wote wa Mamlaka ya Bandari Tanzania kuwa mizigo haitarundikana katika Bandari ya Dar es Salaam, pia huku inakoletwa haitarundikana," alisema.

"Tunategemea wadau mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Mapato (TRA) na wengine waje kufanya logistics za kutoa mzigo kwa haraka na tunategemea kutakuwa na maegesho mengi, hivyo malori yataingia na kushusha mizigo kwa haraka," alisema Nditiye.

Ndikilo alisema mwingiliano wa watu na mali utakuwa mkubwa katika bandari hiyo na jambo la kuzingatia ni kuhakikisha mali za wananchi zinakuwa salama na vyombo vya dola vinafanya kazi kikamilifu.

"Hilo litasimamiwa na vyombo vya usalama wakiwamo Polisi, na najua kuna RPC wa Bandari, lakini itabidi ashirikiane na RPC wa Mkoa wa Pwani ili hali ya amani na utulivu iendelee kuwapo eneo hilo," alisema Ndikilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari, Kakoko alisema Mamlaka ya Bandari, wajumbe na mwenyekiti wa bodi watahakikisha wanamaliza kazi kwa muda uliopangwa na kwa mujibu wa maelekezo ya serikali kupitia wizara, eneo hilo litaanza kufanya kazi rasmi Julai.

# Mitambo kisasa TFS kuzima moto

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umesema katika kukabiliana na majanga ya moto kwenye mashamba ya miti na misitu asili, umejipanga kununua mitambo ya kisasa yenye uwezo mkubwa wa kuzima moto katika kanda zao zote saba nchini.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mtambo wa kuzima moto katika eneo la Ruvu mkoani Pwani ambao umetengenezwa na Kampuni ya Equator SumaJKT, Kamishna Mhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema mtambo huo ni wa kwanza nchini na ni maalum kwa kuzima moto katika mapori na misitu.

Alisema lengo la kuamua kununua mitambo maalum ya kuzimia moto, ni kuhakikisha misitu inalindwa dhidi ya matukio ya moto ambayo yamekuwa yakitokea katika misitu hiyo.

"Moja ya changamoto kubwa ambayo tunakumbana nayo ni misitu kuungua moto na kusababisha hasara kubwa, kwa mwaka 2019 hasara tuliyoipata kutokana na matukio hayo ni Sh. bilioni tano ambayo ni katika shamba moja la miti Sao Hill tu, kwa hiyo kuwa na mitambo ya kuzima moto ni moja ya kipaumbele chetu," alisema Prof. Silayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Equator SumaJKT, Robert Mangazeni, alisema mtambo unahimili mazingira ya aina yoyote, na kwamba una nguvu ya kutumika katika majanga ya moto kwenye misitu, majiji na katika viwanja vya ndege, huku akisema kwa Afrika ni wa kwanza.




Waziri wa Afya, Jinsia ,Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), akipokea msaada wa lita 618 za vitakasa mikono kutoka kwa Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa Kampuni ya TBL, Georgia Mutagahywa (kulia) vilivyotolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya vituo vya afya kupambana na na maambukizo ya corona. Kushoto ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Angelina Ngalula. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchungaji awafukuza waumini kanisani wasiovaa barakoa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MCHUNGAJI wa Kanisa la Tanzania Assemblies Of God (T.A.G), mtaa wa Misongeni Bingwa, Manispaa ya Morogoro, Simoni Musa, alilazimika kuwafukuza waumini wake ambao hawakuwa na barakoa kwenye ibada Jumapili.

Alisema amechukua uamuzi huo baada ya kubaini wanafanya makusudi ya kutochukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

"Nimelazimika kuwafukuza waumini wote ambao hawakuwa wamevaa barakoa, nina amini kuwa watu hawa wanafanya kakusudi kutochukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa virusi vya corona," alisema Musa.

Mchungaji Musa alisema sasa hivi dunia kwa ujumla ipo katika mapambano dhidi ya corona na kwamba watalaam wa afya wamekuwa wakikisitiza watu kujikinga na kuchukua tahadhari ili kuepuka maambukizo.

Alisema tahadhari imeshatolewa kuwa wananchi wanatakiwa kutumia barakoa wanapokuwa kwenye mikosanyiko, hivyo kitendo cha waumini wa kanisa hilo ni utovu wa nidhamu na hawakupaswa kushiriki ibada ya siku hiyo.

"Naomba nisieleweke vibaya kwa kuwa yeyote mwenye akili timamu hawezi kunilaumu kwa kitendo nilichokifanya na kwamba nitaendelea kuwafukuza wote watakaokuwa wakija kwenye ibada bila kuwa na barakoa," alisema Musa.

Mchungaji huyo alisema ni bora ibada ikafanywa na watu wawili wenye kuchukua tahadhari kuliko kuwa na watu 100 ambayo hawatii agizo la kujikinga na janga hilo na watu wa namna hiyo ni wakuogopa kama ukoma.

Alisema yeye ni kiongozi wa dini wajibu wake ni kuhakikisha waumini wa kanisa hilo wanakuwa mstari wa mbele kujikinga na corona kwa kuwa kitendo cha kuchukua tahadhari kitawaelimisha watu wenginye pia nao kujikinga.

Kitendo hicho kimepongezwa na wananchi wa Mkoa wa Morogoro na kuwataka viongozi wengine wa dini kuwahimiza waumini wao kuvaa barakoa wanapokuwa kwenye ibada kwa kuwa maambukizo ya ugonjwa wa corona yapo na yanaua.

Anna Kalugula alisema Watanzania wanatakiwa kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo na kuacha mzaha kwa kile wanachoshauriwa na wataalamu wa afya na kuitaka jamii kuendelea kumuomba Mungu ili aiepushe dunia na janga hilo.

# Wasafiri nchini kunufaika na mfumo malipo ya kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

WASAFIRI nchini wataanza kunufaika na mfumo wa malipo kwa njia ya kidigitali.

Mfumo huo mpya wa malipo kwa njia ya kidigitali kwa wasafiri nchini (EYWA), ulizinduliwa juzi na Kampuni ya MasterCard kwa kushirikiana na kampuni ya utoaji huduma za usafiri - EYWA na Benki ya NMB.

Huduma hiyo ambayo itakuwa ndani ya kadi maalumu za kielektroniki pia watumiaji wa simu za mkononi wataweza kupata taarifa huku watumiaji wa simu rununu (smartphone) watakuwa na uwezo wa kupakua programu maalumu kupata maelezo ya huduma hiyo.

Uwepo wa progamu hiyo itakuwa suluhisho la changamoto za huduma za usafirishaji nchini kwa kupunguza matumizi ya mfumo wa malipo ya fedha taslimu na kuja na mfumo wa malipo kwa njia ya kidijitali kwa mamilioni ya abiria nchini.

Kwa uwezeshaji wa Mastercard QR, EYWA na Benki ya NMB, wasafiri wanaweza kupunguza mawasiliano ana kwa ana na kupata huduma za usafiri kwa njia salama. Huduma hii inawawezesha wasafiri kuacha kupanga foleni za ununuzi wa tiketi; kurudi kuangalia muda wa safari.

Kwa kupitia simu za mkononi na kadi maalumu, wasafiri wataweza kukata tiketi kwa njia ya kidijitali na kupunguza muda wa huduma husika.

Watoa huduma za usafiri au wamiliki wa mabasi kwa upande mwingine wataweza kukagua orodha ya abiria waliofika katika kila kituo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa EYWA, Toffène Kama, alisema: "Tumejitolea kutoa huduma bora za usafirishaji watu wengi kupatikana kwa urahisi na kuwezesha mamilioni ya Waafrika kusafiri salama kila siku, kwa gharama wanazoweza kumudu.

Wakati dunia inakabiliwa na janga la COVID-19, tunafurahi kuzindua huduma hii ambayo itawawezesha wasafiri Tanzania kusafiri huku wakiwa salama kwa kupunguza huduma zinazowalazimu kuonana ana kwa ana kila mara."

"Kupitia Mastercard QR na teknolojia yetu ya kipekee, huduma hii inarahisishaji ukusanyaji wa nauli kutoka maeneo mengi kwa njia mbalimbali katika mfumo mmoja. Ni mfumo rahisi, salama usio na shida kwa madereva na abiria wote," alisema na kuongeza:

"Tunapongeza juhudi za Chama cha Wasafirishaji jijini Dar es Salaam (UWADAR) na juhudi zao nyingine katika kuhakikisha mtandao wao wa madereva unatumia mfumo huu kutoa huduma bora kwa wateja wao."

Mkuu wa Biashara kutoka MasterCard Ukanda wa Afrika Mashariki, Mastercard, Adam Jones, alisema: "Wakati watu wakisafiri zaidi kuelekea katika maeneo ya mijini kwa lengo la kufanya kazi au kupata burudani, mamlaka za miji zinatafuta mfumo rahisi wa pamoja wa usafiri wa umma.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema: "Tumejitolea kukuza sekta ya usafirishaji Tanzania na kufanya kazi na washirika kama EYWA na Mastercard kuanzisha mfumo wa malipo ya kidijitali ambao mbali na kupunguza matumizi ya fedha taslimu pia utakuwa na faida kwa wasafiri au abiria na uchumi kwa ujumla.

"Utaratibu huu wa malipo ni sehemu muhimu ya mikakati ya NMB kutoa mfumo jumuishi wa kifedha kwa watoaji huduma za usafiri na sekta nzima kwa ujumla.

"Kwa kushirikiana na Mastercard QR, tunatoa njia bora kwa wasafiri kupokea malipo kutoka kwa watoaji wa huduma za usafiri na wateja wa benki za kibiashara ambazo zimeunganishwa na huduma za Mastercard QR," alisema Zaipuna.

## HABARI BUNGENI

# Maji ya Mto Ruvuma kutumika vijiji 50 vya mkoa wa Mtwara






Habari na Augusta Njoji

SERIKALI imesema ipo kwenye mpango wa kujenga mradi mkubwa wa maji kutoka kwenye Mto Ruvuma utakaohudumia zaidi ya vijiji 50 vya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba na Wilaya ya Mtwara.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Wizara ya Maji katika swali la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kwa muda mrefu wakazi wa Mji wa Nanyamba wanapata shida kubwa ya maji licha ya kuwa jirani na mto Ruvuma.

"Je, ni lini serikali itaanzisha mradi mkubwa wa maji utakaonufaisha wananchi wa Kata ya Kitaya, Kiromba, Chawi na Mtiniko?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema ipo kwenye mpango huo na mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kupitia fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na kwa sasa upo kwenye hatua za awali za maandalizi.

"Katika kutatua kero ya maji kwa muda mfupi kwa wananchi waishio katika Mji wa Nanyamba na kata za Kitaya, Kiromba, Chawi na Mtiniko, serikali imetekeleza na inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji wakati mradi mkubwa unasubiriwa," ilisema.

Ilieleza kuwa Mji wa Nanyamba ambao una wakazi wapatao 24,021 unapata huduma ya maji kupitia mradi wa Mnyawi.

"Katika kuboresha zaidi huduma ya maji, serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Nanyamba mjini wenye thamani ya Sh. milioni 944.19, ambapo visima virefu viwili tayari vimechimbwa na ujenzi wa mradi huo unaendelea," ilisema.

Pia, ilibainisha kuwa katika kuhakikisha huduma inaboreka zaidi mnamo Januari, mwaka huu Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA), imepewa jukumu la kusimamia huduma zote za maji katika mji huo.

Vilevile, ilisema serikali kupitia Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) ipo kwenye mpango wa kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya Kitaya wenye thamani ya Sh. milioni 350 kupitia programu ya P4R.

"Mradi huo unategemewa kuanza mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Novemba, 2020," ilisema.

# Kamati 16,000 zaanzishwa kulinda wanawake, watoto

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imechukua hatua mbalimbali kukabiliana na ukatili wa kijinsia ikiwamo kuanzisha kamati za ulinzi za wanawake na watoto 16,343 kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kamati hizo zinawajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama wa wanawake na watoto.

Wizara hiyo ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Grace Tendega.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema ukatili wa kijinsia umekuwa ni tatizo kwa sasa nchini. "Je, serikali imejipangaje kutatua tatizo hilo?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema pia madawati ya jinsia na watoto 427 yameanzishwa katika vituo vya polisi.

Ilisema serikali inatambua vipo vitendo vya kuwanyanyasa, kuwadhalilisha na kuwadhulumu vinatafsiriwa kama ukatili ambavyo kwa sehemu kubwa, huwaathiri zaidi wanawake na watoto katika jamii.

"Vitendo vikifanyika kwa mrengo wa jinsia tunaviita ukatili wa kijinsia, serikali imechukua hatua mbalimbali za kuzuia na kutokomeza ukatili huo ikiwa ni pamoja na kuanzisha kwa kamati na madawati hayo," ilisema.



Kadhalika, ilisema jitihada nyingine ni Sheria ya Elimu imefanyiwa marekebisho mwaka 2016 na kuweka adhabu ya kifungo cha miaka 30 kwa kosa la kumpa mimba, kuoa au kuolewa na mwanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Aidha, ilisema serikali imetekeleza sheria ya elimu pasipo malipo kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi ili kuwezesha watoto wa kike na wa kiume kupata elimu bila kujali uwezo wa kiuchumi wa familia.

"Pia sheria ya fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa imefanyiwa maboresho na kufanya uchangiaji wa asilimia 10 kuwa wa kisheria kwa kuwezesha mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi," ilisema.

Wizara hiyo ilisema hatua nyingine ni kutungwa kwa sheria ya msaada wa kisheria Namba 1 ya mwaka 2017.

"Sheria hii inatoa fursa kwa wanawake waliofanyiwa unyanyasaji au kudhulumiwa kupata haki zao kutokana na huduma za msaada wa kisheria kupitia vyombo vya usimamizi wa sheria," ilisema.

Kadhalika, ilisema serikali imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kutokomeza ukatili wa kijinsia.



# Serikali yatoa ufafanuzi ulipaji wa kodi

BUNGE limeelezwa kuwa masuala ya kodi nchini hutozwa na taasisi za kikodi kulingana na sheria za kodi zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Wizara ya Nishati katika swali la Mbunge wa Shaurimoyo (CCM), Mattar Ali Salum.

Katika swali lake, alisema Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) hununua umeme wa jumla kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), lakini wanaponunua umeme hutozwa kodi ya ongezeko la thamani(VAT) na Mamlaka ya Mapato (TRA).

"Na wanapokwenda kuuza Zanzibar hutozwa tena kodi ya VAT na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), jambo ambalo hupelekea shirika hilo kuwa na madeni makubwa, Je, serikali inalijua hilo?" Alihoji.

Mbunge huyo pia alihoji serikali ina mikakati gani ya kuondoa kero hiyo.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema masuala ya kikodi hutozwa na taasisi hizo kulingana na sheria na kwamba pamoja na hali hiyo serikali imeendelea kutatua kero mbalimbali za kikodi katika biashara ya umeme kati ya mashirika hayo.

"Kwa vipindi tofauti TRA na ZRB zimekuwa zikifanya mapitio ya kodi hizo ili kuleta manufaa kwa pande zote mbili za Muungano," ilisema.

Ilieleza kuwa katika hatua ya kupata ufumbuzi wa kudumu katika jambo hilo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi na Ushuru Mbalimbali ya Mwaka 2019/20 ambapo umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar uliondolewa VAT na kubaki asilimia sifuri.

Ilisema katika hatua nyingine, SMT kupitia Wizara ya Nishati na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati zinasimamia kwa karibu majadiliano yanayoendelea kati ya Tanesco na Zeco kuhusu bei ya kuuziana umeme.

"Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura) na Mamlaka ya Udhibiti (ZURA) zinashirikishwa, lengo ni kuhakikisha kuwa biashara ya umeme kati ya Tanesco na Zeco inafanyika kwa ufanisi na kuyanufaisha mashirika hayo yote mawili pamoja na wananchi kwa ujumla," ilisema.

Wizara hiyo ilisema suala hilo limefikishwa katika ngazi za watendaji wakuu wa serikali zote mbili wakiwamo makatibu wakuu.

ama
ALHAMISI MEI 7, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**RC Malima: Hospitali Rufani Mara mbioni, huduma kutikisa**




Ukurasa 13

Shinyanga mguu kwa mguu mapambano kukabili corona



Ukurasa 12

**Mayai: Protini 100%, ubora wa afya yako kwa namna hii**

AFYA

# Ofisa Afya: Saluni, vinyozi kaeni 'standby' na corona

• Barakoa muhimu 'kupita maelezo'

**Na Yasmine Protace**

KATIKA kupambana na maambukizo ya virusi vya corona, sasa ni rasmi kila mmoja anapaswa kuchukua hatua sahihi, ili kuhakikisha anapambana na ugonjwa huo.

Elimu imekuwa ikitolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kutangaza kupitia vyombo vya habari kila mara, jinsi ya kujikinga na virusi hivyo.

Wadau wa sanaa nao wako mstari wa mbele wakitunga nyimbo zenye ujumbe unaoasa kujikinga na virusi corona au Covid 19.

Mtazamo uliopo ni kwamba, elimu inayoendelea kutolewa, itasaidia kukabili vita virusi vya corona vinavyoingia mwilini kupitia mfumo wa hewa na watu kugusana. Katika kupambana na kirusi hicho kwa sasa, inaelezwa kila mwenye duka, saluni, sehemu za biashara mbalimbali kumekuwapo madumu ya maji yanayotumiwa na watu kunawa mikono, kwa ajili ya kujikinga na corona.

Mbali na kunawa mikono, pia wananchi kuvaa barakoa na kukaa katika usafiri 'wakiwa levo siti.' Nayo ni moja ya sababu za kujikinga na virusi vya corona.

Katika kupambana na hali hiyo, baadhi ya watu wamejipatia ajira za muda kwa kuuza balakoa ili waweze nao kujiingizia kipato.

Katika mikakati hiyo, sasa wanaofanya kazi katika madaloni nao wanatakiwa kuchukua hatua pale wanapotoa huduma kwa wateja wao.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, imetoa wito kwa wafanyakazi katika maeneo ya saluni kuchukua tahadhari ili kujikinga na maambukizoya homa kali ya mapafu, inayosababishwa na virusi vya corona katika maeneo yao.



Mtoa huduma katika saluni, akiendelea na kazi, huku akiwa katika kinga ya barakoa. **PICHA: YASMINE PROTACE**

> **Tunawakumbusha muepuke msongamano ndani, awepo mtu anayenyoa na anayenyolewa..**

Mkuu wa Kitengo cha Maji na Usafi wa mazingira, katika wizara hiyo, Anyitike Mwakitalima, alipowaelimisha wakazi wa Dar es Salaam, anatawaka kuchukua tahadhari za kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona.

Anasema, mapambano dhidi ya ugonjwa yanaendelea, hivyo ni jukumu la wananchi kuhakikisha wanafuata elimu ambayo inayotolewa kupambana na janga hilo la Covid 19.

Ofisa huyo wa afya, anawataka wafanyakazi wa saluni wahakikishe wanajilinda kila wanapokuwa wanahudumia wateja wao, akiongeza:

"Kwa wale ambao wanaosafisha nywele, kucha, wanafanya masaji, wanaosuka nywele, mchukue tahadhari, kwa sababu mpo katika hatari kubwa sana ya kuambukizwa, lakini vile vile kuambukiza watu wengine," anasema

Anyitike, anasisitiza haja ya serikali kuendelea kuwakumbusha wafanya kazi katika maeneo ya saluni, wahakikishe wanaepuka msongamano, pindi wanapokuwa katika majukumu yao, pasipo kusahau vazi la barakoa, pindi wanapohudumia nywele za wateja wao.

Pia, ana ushauri kwamba saluni nyingi zina kawaida ya msongamano ya watu mbalimbali wanaofika mahali hapo kupata huduma mbalimbali, hivyo ni wajibu wao kuzingatia misingi ya elimu dhidi ya virusi vya corona.

"Tunawakumbusha muepuke msongamano ndani, awepo mtu anayenyoa na anayenyolewa na yule ambaye ananyoa, ahakikishe muda wote amevaa barakoa. Tunawaambia hivi kwasababu tunawapenda" anasema.

Pia, askari Polisi wa Usalama Barabarani, Staff Sajenti Valentine Ngowi, anawataka madereva wa vyombo vya moto, hususan bodaboda na bajaji kuhakikisha wanavitakasa vyombo vyao vya usafiri kwa sabuni kila mara, kuepuka maambukizo ya virusi vya corona, kama njia ya kujihami kwa tahadhari.

Balozi wa Kampeni ya 'Mikono Safi, Tanzania Salama,' msanii Mrisho Mpoto au maarufu 'Mjomba' anasisitiza kwamba katika kupambana na ugonjwa huo, watu wasichoke kunawa mikono kwa sabuni na maji safi yanayotiririka, waepuke maambukizo ya virusi vya corona.

Mpoto anasema, kila mmoja akifuata maelekezo yanayotolewa kuhusu kujikingana na virusi hivyo, basi atakuwa katika hatua ya mafanikio dhidi ya vita hiyo, huku mkazi wa Dar es Salaam, Jumanne Jabiri, anaitafsiri kuwa 'kampeni iliyokuja kwa wakati.'

Kwa mujibu wa Jabiri, wasusi na vinyozi walioko katika vijiweni mitaani, wamepata elimu na sasa wanapaswa kuhama kutoka katika utendaji wa mazoea ya kazi na kuwa katika mazingira ya kujikinga zaidi kiafya, wanapokuwa kazini.

Ni uhamasishaji unaofanywa kupitia kampeni ya 'Mikono Safi, Tanzania Salama" inayoendelea jijini Dar es Salaam, chini ya uratibu wa wizara inayohusika na afya nchini, kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Project Clear kwa kushirikiana na Msanii Mrisho Mpoto na Mjomba Theatre Gallery, anakotoka Mpoto,.

AFYA

# Mayai: Protini 100%, ubora wa afya yako kwa namna hii

• Tiba mifupa, nywele, kucha, sumu, macho, ubongo wa wazee & watoto



Mlo wa yai la kuchemsha. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Mayai ya kukaanga yakiwa na mkate.

**Na Mwandishi Wetu**

MARA nyingi iko wazi hasa vijana na zaidi watoto wanapenda sana mlo mayai. Msingi wa mvuto wao uko katika ladha zaidi na hata pale wanapoangukia kwa simulizi za 'chipsi mayai' au 'mayai kwa mkate' hasa kwa jamii za Magharibi .

Ni lishe ambayo inatoka kwa kiumbe kuku zaidi na kundi la jamii ya ndege na wanaofanana nao kama vile bata. Inapokuwa mlo, uandaaji wake unaweza kuwa wa namna nyingi, lakini kuu iko katika makundi mawili, ya kukaanga na kuchemsha, ingawaje wapo wachache wanakula hata mabichi.

> **Mayai yanaelezwa tena kwa nafasi kubwa yanapunguza madhara yanayotokana na kuchakaa mboni na lensi ya macho, ikiwamo matokeo ya umri wa mwanadamu.**

### SIFA ZAKE

Kwa kurejea wasifu wa kitaalamu kutoka kwa wataluma wa Farmers Market, mayai yanamsaidia mtumiaji kuhisi mwenye shibe kwa kipindi kirefu. Hiyo ni kutokana na kila yai kuwa na uwezo kumpatia malaji protini yenye ubora na virutubisho mbalimbali muhimu vinavyohitajika mwilini, isipokuwa vitamin C.

Hapo wanaeleza ndio kiini cha ushauri kwamba kila yai linapaswa kuliwa kwa kujumuishwa na walau matunda au juisi ya machungwa, pia mkate uliotayarishwa kwa unga kumwezesha mtumiaji kuwa katika hali nzuri zaidi kiafya.

Pia, ina nafasi ya kumuondolea mlaji upungufu wa madini ya chuma mwilini, pale anapohisi dalili mbalimbali za uchovu, kuumwa vichwa na kuwashwa ngozi.

Ni madini yanayobeba hewa ya oksijeni kwenye damu na hufanya kazi muhimu katika kuimarisha kinga za mwili na usanisishaji wa nishati mwilini.

Aidha, madini ya chuma yanayopatikana kwenye kiini cha yai, yako katika mfumo ulio tayari kufyonzwa na kutumika mwilini, kuliko aina ya chuma zinazopatikana kwenye virutubisho vingine vya vyakula.

Idadi ya virutubisho vilivyomo kwenye mayai, inaelezwa inayafanya kuwa na mchango muhimu kwenye lishe ya mlaji. Kuna utafiti uliofanywa baina ya walaji mayai na wasiotumia, ulibaini wasiotumia mayai wanaangukia katika upungufu mkubwa wa viinilishe; vitamini A, E na B12.

Msingi wake kitaalamu ni kwamba mayai yanachangia mwilini kiasi cha asilimia 10 hadi 20 cha madini aina ya folate na kiasi cha asilimia 20 hadi 30 cha vitamin A, E na B12 kwa watumiaji wake.

Hali kadhalika, licha ya katika miaka ya 1990 kuwapo watafiti waliotangaza vibaya kuwa na lehemu, zipo tafiti kinazani zilizofuatilia na kuyatetea mayai kwamba hayana uhusiano na ongezeko la lehemu mwilini, hata kumfikisha mlaji katika magonjwa ya moyo.

Pia, mtu anapotaka ama kudhibiti uzito wake au kuupunguza, basi mayai yana nafasi kama lishe mbadala, kwani hata utafiti mbalimbali umekuja na uthitibitisho huo kutoka kwa walaji wa mayai

Eneo lingine la faida ya ulaji mayai, inashuhudia katika afya ya ubongo. Ni kirutubisho kinachojulikana kama choline, kinachosaidia kuboresha ubongo na hasa kwa watoto wadogo, pia wazee.

Kwa mama majamzito naye ana faida ya kirutubisho choline, kila anapokula walau yao moja kwa siku, kwani inamnufaisha kirutubisho hicho cha choline, kwa wastani wa asilimia 28. Ni kirutubisho muhimu sana hata wakati wa mama kunyonyesha, akiba yake ya kirutubishi inapokuwa imepungua na ni wakati muhimu sana kwa ukuaji wa ubongo wa mtoto na uboreshaji wa kumbukumbu yake atakayodumu nayo.

Katika eneo la uwezekano wa mtu kupatwa na magonjwa yanayohusiana na macho, mayai tena yanachukua nafasi ya kuwa na maboresho yake Ulaji mzuri wa mayai, pamoja na mboga kama spinachi kwa kiasi kikubwa, ni msaada mkubwa katika kuyakinga macho, dhidi ya magonjwa ambayo vinginevyo yanamuweka mhusika pagumu.

Mayai yanaelezwa tena kwa nafasi kubwa yanapunguza madhara yanayotokana na kuchakaa mboni na lensi ya macho, ikiwamo matokeo ya umri wa mwanadamu.

Pia, imedumu kuwa chanzo muhimu cha kuondoa baadhi ya sumu mwilini (antioxidants) zinazofanya kazi muhimu ya kuhakikisha macho ya binadamu, yanadumu kuwa salama.

Vyanzo hivyo kwa kawaida, hukusanyika kwenye macho kuyalinda dhidi ya miale mikali ya mwanga, yenye madhara makubwa na hivyo, kula mayai tangu umri mdogo, ni kujihakikishia kupata virutubisho na kujiepusha na upofu.

### BINGWA PROTINI

Ikiwa ni chanzo kikuu cha protini mwilini, sehemu ya aina kuu tatu ya vyakula inayojenga mwili, ikihusika kwenye ujengaji na ukarabati wa chembechembe na tishu mbalimbali za mwili. Mayai yanapewa nafasi ya bingwa wa kusambaza protini hizo muhimu mwilini.

Tindikali za amino (amino acids) ndiyo matofali yanayojenga protini hizo na kwa bahati mbaya miili ya binadamu, haina uwezo wa kuzalisha tindikali hizo, ni lazima zipatikane kupitia vyakula. Kwa maana hiyo, kula mayai husaidia kukua kwa mwili na kutunza chembechembe hai na tishu za miili yetu. Kwa mfano, mayai, maziwa na nyama, zote ni protini zilizo kamili na bora.

Lakini, mayai yanabaki bora zaidi kwa sababu yana portini asilimia 100; maziwa asilimia 93 na nyama ya ng'ombe au samaki asilimia 75.

Inakadiriwa kitaalamu kila yai moja, lina kiwango sawa cha protini na gramu 30 za nyama ya ng'ombe, samaki au kuku iliyopikwa.

### NYWELE, KUCHA, MIFUPA

Wataalamu wanaainisha kwamba ni chanzo cha vitamini D na kwa maana nyingine, ni muhimu kwa kwa madini ya calcium mwilini, ili kuimarisha afya za mifupa. Hivyo mayai na maziwa vinasaidia kuepuka tatizo la mifupa mwilini au hata udhaifu wake kuvunjika kirahisi.

Mayai husaidia kuboresha afya ya nywele na kucha kwa sababu ya kuwa na tindikali za amino zenye wingi wa madini ya salfa na wingi wa vitamini na madini mengine.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za utaalamu wa lishe na afya.***

AFYA

## WAKATI KUNA HODI YA MAAMBUKIZO...

# Shinyanga mguu kwa mguu mapambano kukabili corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

•RC, ma-DC waonya mzaha • Asasi mkoa zajiunga kampeni



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (wa pili kutoka kushoto), akipokea msaada wa ndoo za kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, zitakazosambazwa kwenye maeneo ya huduma za jamii. **PICHA: MARCO MADUHU.**

HALI si nzuri katika kuendeleza mapambano ya kujikinga dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona nchini, uongozi wa kiserikali katika mikoa mbalimbali unaedelea kuchukua hatua za kuelimisha wananchi.

Pia, wadau wa aina mbalimbali, nao wanaendelea na kazi ya utoaji misaada ya vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo, ikizingatiwa

Sehemu ya nyenzo muhimu dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona mara mtu anapokuwa katika mkusanyiko wa umma, ni kwamba anawe kwa sabuni na maji tiririka, au kupata huduma za vitakasa, pia kujihami usoni kwa barakoa.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, anasema rai yake kwa wakazi ni wajilinde dhidi ya mabumbukizo.

Anaendelea kwa kauli kali: "Kwa wale ambao wanaendekeza mzaha kwenye mapambano ya kujikinga na virusi hivi vya corona, tutawachukulia hatua pamoja na kuwapiga faini.

"Pia, natoa onyo kwa wananchi ambao wanafanya mzaha wa kupiga simu kwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, na kudanganya kuwa wana virusi hivyo kumbe hawana tabia hii ife.

"Janga hili ni hatari siyo la kufanyia mzaha, bali kila mmoja achukue tahadhari pamoja na kufuata maelekezo ya serikali ndipo tutabaki salama."

Mkoa wa Shinyanga ulitangazwa kupata wagonjwa wapya wawili mwishoni mwa wiki iliyopita, ikiwa ni siku chache tangu kupatikana misaada kadhaa iliyotolewa kutoka asasi mbalimbali kimkoa, katika juhudi za kujihami dhidi ya maradhi ya corona, kabla hayajaingia.

### BOSI SHUWASA

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji, Usafi na Mazingira, mjini Shinyanga (Shuwasa), Flaviana Kifizi, katika ziara yake kukagua maeneo mbalimbali ya jamii, kukagua mwitikio wa wananchi dhidi ya tahadhari ya kinga na maambukizo anaeleza kubaini changamoto.

Ikiwa ni sehemu ya kutekeleza maelekezo ya mkoa kwa matendo, Kifizi anataja kugundua mzaha dhidi ya maagizo, ukiukwaji kanuni na maelekezo sahihi ya kitaifa, ikiwamo ukiukwaji matumizi ya ndoo zisizo zenye vigezo kwa ajili ya kunawa.

Kifizi anaukumbusha umma tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, huku wengine ndoo zikiwa tupu hazina maji ndani.

"Shuwasa tunaungana na serikali kuendeleza mapambano ya kudhibiti maambukizo ya virusi vya Corona," anasema Kifizi.

> **Janga hili ni hatari siyo la kufanyia mzaha, bali kila mmoja achukue tahadhari pamoja na kufuata maelekezo ya serikali ndipo tutabaki salama.**



Nyabaganga Talaba, Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, akinawa kwa vitakasa mikono, kabla ya kutembelea mgodi wa dhababu wilayani kwake. **PICHA: MTANDAO.**

### VIONGOZI WILAYA

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, anakiri kasoro zilizotajwa kuhusu kuwepo mzaha kwa kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Anataja mahali husika, panajumuisha vijiwe vya bodaboda, vilabu vya pombe, baa na kumbi za starehe, ambako kuna mlundikano wa watu na ukosefu wa vifaa vya kunawa na sabuni.

Macha anawakumubsha wananchi wakazo wake kuchukua tahadhari, wakianza na kuweka kando mzaha penye mwingiliano wa umma, hasa kutoka maeneo yaliyoathirika, akitaja mfano wa nchi jirani kama Rwanda, Burundi na Jamhuri wa Kidemokrsia Congo (DRC).

Aidha, jirani yake Jasinta Mboneko, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, anawaagiza maofisa watendaji wa kata na afya, wafanye ukaguzi kuzunguka maeneo ya kijamii yanayoweka ndoo tupu zisizo na maji, ili wahusika wachukuliwe hatua kisheria, kwa kupuuza maelekezo ya serikali.

Mboneko anasema, serikali ilishatoa maelekezo kila penye huduma za kijamii, panapaswa kuwekwa ndoo bora zenye maji ndani yake, ili wananchi wanawe mikono kwa sabuni na majitiririka, kabla ya kupata huduma, ili wajikinge dhidi ya maambukizo ya virusi corona.

"Msaada huu wa ndoo 15 ambazo tumezipokea kutoka kwenye mamlaka ya maji na usafi wa mazingira Shinyanga (Shuwasa), tutazipeleka zote kwenye maeneo ya Sokoni ili kuongeza nguvu ya wananchi kunawa mikono kwa sabuni na Majitiririka, maeneo ambayo yana msongamano wa watu wengi,"anasema Mboneko na kuongeza:

"Matenki haya mawili ambayo na sisi tumepewa na mgodi huu wa madini ya dhahabu Barrick tuta yapeleka kwenye maeneo ya Standi ya Mabasi, ambapo napo kuna msongamano wa watu wengi, lengo likiwa ni kuongeza nguvu ya kupambana na maambukizo haya ya virusi vya Corona hapa Shinyanga."

### WADAU MIGODI

Kampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu, Barrick, kupitia mgodi wake wa Buzwagi, wilayani Kahama, umo katika orodha ya wadau wa Shinyanga, wanaoungana na serikali, kuendesha mapambano dhidi ya kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona.

Antoinette George, ni Mkuu wa Kitengo cha Afya na Usalama Kazini kwenye mgodi wa, Barrick- Buzwagi, anasema nao wameamua kujiunga na kundi la wadau wa vita dhidi ya Covid 19, kwa kuchangia vifaa vya kujikinga dhidi ya virusi hivyo.

Anataja walivyochangiana idadi yake: Barakoa 400, glovu jozi 50; vipima joto saba; dawa aina ya klorini kilo 45; matenki ya maji 88; na mavazi maalum madaktari wakati wa kutibu wagonjwa wa corona suti 40.

### VIONGOZI WILAYA

Mkurugenzi (DED) wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, anasema ili kuunga juhudi za wadau katika kutoa msaada wao wa vifaa vya kupambana na maambukizo ya virusi vya Corona, atalazimika kuweka askari mgambo katika maeneo ya soko na standi za mabasi, kuwasimamia wananchi kunawa mikono kwa lazima.

AFYA

## MIAKA 43 YA KUSUBIRI...

# RC Malima: Hospitali ya Rufani Mara mbioni, huduma kutikisa

**Na Sabato Kasika**

NI simulizi inayochukua miaka 40 na kadhaa, leo hii kunatekelezwa wazo la Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, kujengwa Hospitali ya Rufani Mkoa Mwanza, katika kitongoji cha Kwangwa ndani ya Manispaa ya Musoma.

Mkuu wa Mkoa, Adam Malima, anasema ni uamuzi uliorejeshwa tena katika utekekezaji kupitia mikakati ya kufufua mipango mbalimbali ya Mwalimu Nyerere.

Ni mradi unaoatarajiwa kunufaisha wakazi kutoka wilaya za Butiama, Rorya, Tarime, Musoma Mjini, Musoma Vijijini na Serengeti, pia majirani na wageni wao.

Pia, Manispaa mjini Musoma, ambako kwenye mradi unaotekelezwa kwa jina la Mwalimu Nyerere Memorial Hospital, ulioko katika mwambao wa Ziwa Victoria.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, anasema hospitali hiyo inajengwa katika eneo lililopo mbali wa kilomita mbili, Kusini mwa mjini Musoma, kwenye mwinuko ukipambwa na madhari ya Ziwa Victoria.

Anasema, ujenzi wa hospitali hiyo ulianza mwishoni mwa mwaka jana, baada ya Rais Dk, John Magufuli, kuidhinisha zaidi ya Sh. bilioni 15.

Malima anasema, ni ujenzi unaofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na tangu kazi hiyo ianze, kuna hatua kubwa iliyopigwa kupitia mradi. Mkuu wa Mkoa anasema mipango waliojiwekea ni hadi kufikia Julai ijayo, ujenzi uwe umekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa mkoani, hata wageni wa nchi jirani.

"Hospitali hii haitakuwa ya Rufani ya Mkoa, bali itakuwa ya kibingwa na kibobezi kwa baadhi ya huduma na itatoa huduma kwa wananchi wote wa Kanda ya Ziwa," anajigamba Malima, huku akiwataja wa mikoa na nchi jirani nao ni wanufaika.

"Kukamilika hospitali hii itakuwa mkombozi kwa wananchi wa mkoa wa Mara ambao watakuwa wakipata huduma za hospitali ya rufani katika mkoa wao tofauti na sasa wanalazimika kwenda Bugando, Mwanza," anaongeza.

### SAFARI YA UJENZI

Malima anasema, ujenzi wake ulianza na mkakati wa pamoja kimkoa katika vikao vya pamoja na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Anawataja washiriki wengine aliokuwa nao ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na wawakilishi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), ambao ndiyo makandarasi.

Pia, anamtaja mwakilishi wa Chuo Kikuu cha Ardhi ambaye ndiye Mshauri Mwelekezi katika mradi huo na maofisa waandamizi wa serikali.

"Baada ya kikao hicho kazi ya ujenzi inafanyika usiku na mchana kuhakikisha hospitali inakamilika haraka, ili kuhakikisha huduma zinaanza kutolewa kwa muda uliopangwa," anasema.



Jengo jipya la Hospitali ya Mkoa Mara, ujenzi wake ukiendelea. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

> **Kukamilika hospitali hii itakuwa mkombozi kwa wananchi wa mkoa wa Mara ambao watakuwa wakipata huduma za hospitali ya rufani katika mkoa wao tofauti na sasa wanalazimika kwenda Bugando, Mwanza.**



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima.

Mkuu huyo wa Mkoa anasema, jengo la hospitali hiyo limepitia kwa makandarasi wawili, kabla ya NHC kukabidhiwa kazi na limefanyiwa maboresho, ili kuwa na huduma zote za kiwango cha hospitali za rufani.

Mkuu wa Mkoa anasema, katika kufanikisha mradi kumekuwapo ziara za kila mara zinazofanywa na viongozi wa kiserikali kukagua na kusaidia kutatua changamoto zinazoukabili mradi, ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

Malima anasema, ni hospitali ya ghorofa tano, ikichukua eneo kubwa la mita za mraba 24,482 na majengo mengine ya pembeni yenye mita za mraba 1,039, yaliyogawanyika katika sehemu kuu tatu

### MPANGO AFYA

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Afya (MMAM) ulioanza kutumika miaka 12 iliyopita, kila kijiji au mtaa kwa mijini, kunapaswa kuwepo zahanati na kata kuwa na kituo cha afya.

Vivyo hivyo inaelekeza kwamba, katika ngazi ya wilaya kunatakiwa kuwapo hospitali na mikoa, hospitali zake sasa zitakuwa za rufani na juu yake katika ngazi ya kanda, kama ilivyo Bugando na Mbeya na Muhimbili imekuwa ya taifa.

Hata hivyo, katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, hospitali za manispaa; Temeke, Amana iliyopo wilayani Ilala na Mwananyamala (Kinondoni), zimekuwa za rufani katika hadhi inayofanana na mikoa.

Pia, bado malengo hayajatekelezwa kukidhi wastani wa mahitaji ya mpango MMAM kitaifa, kama ilivyokuwa katika mkoa Mara.

Katika baadhi ya mikoa, serikali kihistoria imekuwa ikiingia katika ubia na hospitali binafsi, hususan na taasisi za kidini na kuwa wawakilishi wa serikali, hivi sasa katika ngazi mbalimbali za MMAM, mpango wenye zaidi ya miaka 10 sasa.

### SERA INAVYOELEKEZA

Sera ya Afya nchini, inafafanua kwamba hospitali nchini zinapaswa kupatiwa vifaa vya hali ya juu, ziweze kutibu magonjwa yote ambayo hivi sasa yanapelekwa watu nchi za nje kwa tiba ya ziada.

Pia, inahimiza umefika wakati hospitali hizo kuwa na 'ubingwa maalum'na katika hilo hospitali ziteue'ubingwa' kuendana na vifaa vya kuhudumia ubingwa huo, kupunguza safari za kupeleka wagonjwa nje.

Lingine, ni hospitali hizo zinahitaji wodi nyingi, kutosheleza mahitaji ya ubingwa maalum, ikiwa ni pamoja na huduma za dharura na uangalizi maalum (ICU).

Pia, inaelekeza hospitali ya rufani kuwa na vitanda kati ya 400 na 600 na wakati wa andiko la sera hiyo, hospitali za rufani nchini zilikuwa na vitanda kati ya 420 na 1,425.

"Ngazi hii iwe na mchanganyiko wa wataalamu wenye taaluma za hali ya juu kabisa, ili kuweza kutekeleza barabara majukumu mengi ya kutoa huduma za tiba na kinga, kufundisha na kufanya utafiti," inafafanua sera hiyo.

Pia, inagusia wigo wa vinavyotakiwa kupatikana katika hospitali za rufani ni: Tiba za kawaida, lakini kwa weledi wa juu; mafunzo ya wataalamu wapya na wa kujiendeleza; kufanyika utatifi; utoaji ushauri wa kitaalamu kuhusu afa nchini; kutembelea hospitali nyingine katika kanda (out-reach) ili kutoa ushauri wa karibu na mafunzo kwa wataalamu wa huko.

"Hospitali za rufani zitahitaji vyombo vingi vya usafiri kuliko hospitali za mikoa, ili kuwawezesha wataalamu wa hospitali hizo kutekeleza majukumu yao," inaeleza sera hiyo.





# Femata yajivunia mambo 5 ya JPM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (Femata), John Bina, ametaja mambo matano ambayo wachimbaji wanajivunia katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Rais, John Magufuli.

Miongoni mwake ni kupunguzwa kwa mzigo wa kodi zilizokuwa kero kwa wachimbaji.

Mengine ni wazawa kupewa maeneo ya uchimbaji, kupunguzwa kwa kodi, uanzishaji wa masoko, kugawanywa kwa wizara na kuweka mazingira rafiki ya uchimbaji nchini.

Akizungumza jana na Nipashe, Bina alisema mapinduzi yaliyopatikana hayajawahi tokea tangu Tanzania ipate Uhuru, na kwamba Rais Magufuli ameonesha njia sahihi ya uchimbaji na wanajivunia kwa kuthamini sekta ya madini.

"Ametujengea shime Watanzania ili kuwa mchimbaji si lazima uwe mzungu, na kukaa na sisi kumweleza kero zinazoikabili sekta ya madini ikiwamo kodi, zilizokuwa nyingi na imetolewa Kodi ya Ongezeko la Thamani(VAT) kwenye madini na kwa jumla tumebaki na kodi asilimia saba pekee," alisema.

Kuhusu masoko, alieleza kuwa Tanzania ilikuwa imeingia kwenye kashfa duniani kwamba kuna dhahabu feki na baada ya masoko kupatikana yameleta imani kwa wageni na kupata soko la uhakika kwa wachimbaji.

"Jingine ni Watanzania kupewa maeneo mazuri ya uchimbaji, huko nyuma Watanzania mambo mengi yalikuwa yameshikiliwa na wazungu," alisema.

Alitaja jambo la tano ni kugawanywa kwa wizara badala ya kuwa Nishati na Madini imebaki Madini peke yake, hivyo kurahisisha usimamizi ikiwamo kuundwa kwa Tume ya Madini.

"Kikubwa kinachojumuisha hayo yote ni mapinduzi ya kikodi kutoka Sh. bilioni 170 hadi zaidi ya Sh. bilioni 400, wachimbaji wamelipa kodi vizuri, sisi tunamwombea Rais maisha marefu na wakati fulani nilitoa wazo langu kwamba ingekuwa ni mimi ninayeamua Rais angeendelea kuwa wa kudumu kama China," alisema.

Bina alishauri kutokana na utendaji wa Rais ni vyema uchaguzi mkuu usiwapo na badala yake fedha hizo zielekezwe kwenye uchimbaji ili kuendelea kupaisha uchumi wa nchi.

"Tukiangalia hivi sasa na masuala ya ugonjwa wa corona fedha za uchaguzi zingetumika kununua vifaa vya uchimbaji, yaani kutokana na mtikisiko wa corona, kitakachobaki kuangalia Watanzania ni kilimo na madini pekee na ndio kitatutoa," alisema.

# Shirika laokoa bil. 1/- kwenye dawa za kulevya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI isiyo ya kiserikali ya kupambana na dawa za kulevya (MEFADA), imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 1 kwa mwaka ambazo zinatumiwa na waraibu kununua dawa hizo na kujidunga.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Alex Chitawala, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu namna gani wanavyopambana kuzuia utumiaji wa dawa za kulevya nchini.

Alisema kiasi hicho kilikuwa kikitumika kila mwaka na waraibu hao kununua dawa ya heroin na mabomba ya sindano kwa ajili ya kujidunga.

"Kwa kweli tuna kazi kubwa sana kwa sababu wanaotumia dawa hizo ni watu wenye akili nyingi, uwezo na ubunifu wa kufanya mambo mbalimbali, lakini wameathirika," alisema Chitawala.

Aidha, alisema wamejitahidi kuwahudumia watu hao, ikiwamo kuwapa ajira pale tu wanapopata nafuu ili kuendelea na tiba na kuacha kukimbilia vijiweni.

Alisema Mefada hivi ipo katika mikoa mitatu ya Dodoma, Dar es Salaam na Pwani, kwamba wamejipanga kusambaa katika mikoa mingine nchini ili kutokomeza utumiaji wa dawa hizo.

"Dodoma walikuwa na waathirika wa dawa za kulevya 380, wakati Dar es Salaam ni zaidi ya 1,000 ambao wamepona na wanaendelea na shughuli za ujasiriamali," alisema.

Aliongeza: "Kwa mwezi fedha za dawa na mabomba ya sindano zinazotumika ni Sh. milion 171 ambazo wangeweza kutumia katika kufanya shughuli nyingine za maendeleo ya Taifa."

Hata hivyo, alisema kwa sasa wanatoa elimu kwa waathirika hao, ambao wanawafundisha kutengeneza sabuni za kuwania mikono vitakasa mikono

pamoja na ndoo za maji ambazo zinatumika kwa ajili ya kunawia mikono ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

Kadhalika, Chitawala alisema wanazunguka katika wilaya za Jiji la Dodoma kwa ajili ya kutoa elimu juu ya madhara ya utumiaji wa dawa hizo, na kuwataka vijana kuacha na kujikita kwenye shughuli za maendeleo.

"Tunataka kuona vijana wanafanya kazi na si kutumia dawa za kulevya kama mtaji, kitu ambacho hakikubaliki hata kidogo kwa sababu tunapoteza nguvu kazi ya Taifa," alisema.



Mchuuzi wa mihogo akisaka wateja katika Mtaa wa Bonanza, Chamwino, jijini Dodoma jana. Mihogo hutumiwa katika maandalizi ya futari, hasa kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: PETER MKWAVILAA**

# 'Marufuku wanunuzi wa nje wa mazao kununua kwa wakulima'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amepiga marufuku wafanyabiashara wa nje ya nchi pamoja na kampuni zinazojihusisha na ununuzi wa mazao moja kwa moja kwa wakulima nchini.

Hasunga, aliyasema hayo jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uuzaji wa mazao kwa wakulima nchini kupitia mfumo wa stakabadhi gharani.

Alisema pamekuwapo na wafanyabiashara pamoja na kampuni kutoka nje ya nchi, ambazo zimekuwa zikiingia katika mikoa mbalimbali kutaka kununua mazao moja kwa moja kwa wakulima vijijini.

"Ni marufuku mfanyabiashara kutoka nchi ya jirani kununua mazao moja kwa moja kwa mkulima kijijini, bali wanachotakiwa kufanya ni kusubiri kununua katika soko la upili (Secondary Market)," alisema Waziri Hasunga.

Aidha, alisema kuhusu uuzaji mazao kwa mfumo wa stakabadhi gharani wakulima wanatakiwa kuuza mazao yao kupitia vyama vya ushirika vilivyopo katika maeneo yao.

"Lakini kama hakuna vyama vya ushirika katika maeneo yao wakulima waachwe wauze mazao yao kwa wafanyabiashara wa ndani ambao pia wana leseni za halmashauri husika na wanalipa kodi mbalimbali za serikali," alisema Hasunga.

Pia alitoa onyo kwa viongozi ambao wamekuwa wakiwalazimisha wakulima kuuza mazao yao katika vyama vyao kwa mfumo wa stakadhi gharani.

"Unakuta mkulima ana debe tano unataka auze kwa mfumo wa stakabadhi gharani wakati yeye anahitaji fedha kidogo tu kwa ajili ya kula, lakini wengine hivi sasa wanakusanya karanga za watu wanaweka katika maghara zikipata sumu kuvu hiyo hasara atarudisha nani," alihoji Hasunga.

Vilevile, alisema serikali hajafunga mipaka ya nchi ili kuwawezesha wakulima wake na wafanyabiashara wa mazao ya ndani ya nchi kuuza katika maeneo wanayoyataka na kwa bei itakayowafaa.

Hata hivyo, kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona nchini, Hasunga, alisema kuwa agizo lililotolewa na serikali kuhusu kupiga marufuku mikusanyiko na mikutano katika vyama hivyo vya ushirika bado lipo palepale.

"Bado vyama vya ushirika vinaelekezwa kuwa zuio la mikutano yote ndani ya vyama hivyo vya ushirika lipo palepale, lakini Bodi za Vyama vya Ushirika zinaelekezwa kuomba kibali cha kukasimu madaraka ya mkutano mkuu kwa Mrajis ili ziweze kupitisha baadhi ya maamuzi ikiwamo bajeti za vyama kwa niaba ya mkutano mkuu," alisema Hasunga.

# Wizi, ubadhirifu watishia uhai vyama vya ushirika

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

VITENDO vya wizi na ubadhirifu wa fedha kwenye vyama vya ushirika ni miongoni mwa changamoto kubwa, hivyo kutishia uhai wa baadhi ya vyama hivyo mkoani Mbeya.

Kauli hiyo imetolewa na Mrajisi Msaidizi wa vyama vya ushirika mkoani Mbeya, Angela Maganga, na kwamba mbali na kuwapo kwa changamoto hizo, ofisi ya ushirika kwa kushirikiana na vyombo vya dora likiwapo Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), wamekuwa wakiendesha msako katika vyama hivyo na kuwachukulia hatua viongozi wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya wizi na ubadhirifu wa fedha za wananchi.

Alisema mkoa huo una jumla ya vyama vya ushirika 513 na kuwa kati ya vyama hivyo, na kuwa vyama 408 vinaendelea vizuri na 105 vipo katika hali mbaya kutokana na kutofanya vizuri kwenye ushirika.

Alisema wameanzisha mpango madhubuti wa kutoa elimu kwa viongozi wa vyama vya ushirika juu ya uendeshaji bora, ambapo kazi ya kutoa elimu inafanywa na maofisa kutoka ofisi ya ushirika, Jeshi la Polisi, na ofisi ya ushirika inahusika na ukaguzi wa nje pamoja na wataalamu wa chuo cha ushirika.

"Kuna mpango wa kutoa elimu kwa viongozi wa vyama vya ushirika ili kuwasaidia kuwajengea uwezo wa kuzingatia miongozo bora ya kusimamia vyama vya ushirika kwa ajili ya manufaa ya wanaushirika wote," alisema.

Alisema viongozi wengi wa vyama vya ushirika wamekuwa wakishindwa kufuata miongozo bora ya ushirika katika kuviendesha vyama kwa ufanisi.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahindi (kulia), akikagua ukarabati wa daraja la Mto Piti katika Kijiji cha Bitimanyanga juzi, ambalo lilisombwa na maji na kusababisha mawasiliano kati ya mikoa ya Mbeya, Tabora na Singida kukatika. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Polisi yatoa elimu corona vituo vya daladala, bajaji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

JESHI Polisi mkoani Mbeya, limepiga kambi katika vituo vya mabasi, daladala na bajaji kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuvaa barakoa kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mwishoni mwa wiki kuwa zoezi hilo ni la kawaida kwa kuwa Jeshi la Polisi haliko nyuma katika kuhakikisha abiria wanakuwa na elimu ya kutosha ya kujikinga na maambukizo.

Alisema jeshi hilo limeshakutana na wamiliki na madereva wa vyombo vya usafiri na kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuvaa barakoa katika vyombo vya usafiri.

Alisema ameshatoa maelekezo kwa wakuu wa vituo vyote vya polisi wilaya kuhakikisha wanatoa maelekezo kwa askari hususan wa usalama barabarani kuweka utaratibu wa kutoa elimu kwa abiria kuvaa barakoa.

Alisema Jeshi la Polisi limekuwa likipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya abiria kuwa kuna abiria wengine hawavai barakoa na wamekuwa wakikohoa na kupiga chafya bila utaratibu unaoelekezwa.

Matei alisema wanaendelea na ukaguzi wa baadhi ya mabasi, daladala na bajaji ambazo zimekuwa zikijaza abiria bila kufuata utaratibu na maelekezo ya kitaalamu kuhusiana na maambukizo ya virusi vya corona.

"Lile agizo tulilolitoa kwa madereva kutokujaza abiria tunaendelea kulisimamia na kulitekeleza, na yeyote atakayekamatwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ili liwe fundisho kwa madereva wengine ambao hawatii sheria na maagizo ya Jeshi la Polisi," alisema Matei.

Kamanda Matei ametoa wito kwa abiria na madereva kuzingatia maelekezo ya kitaalamu katika kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona ikiwapo kuvaa barakoa muda wote wanapokuwa kwenye vyombo vya usafiri.

# Wanyama waliotoweka waanza kurejeshwa Hifadhi Taifa Kitulo

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

UONGOZI wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, umeanza kuwarejesha wanyama waliokuwa wametoweka ndani ya hifadhi hiyo kwa miongo kadhaa.

Wanyama hao walitoweka kutokana na shughuli za kibinadamu zilizokuwa zikifanyika kabla ya eneo hilo kupewa hadhi na kuwa hifadhi ya Taifa.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa Kitulo, Susan Tesha, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na jitihada zinazofanywa na uongozi wa hifadhi hiyo kwa nyakati tofauti katika kuhakikisha wanyama wote waliokuwa wanaishi katika eneo hilo wanarejeshwa.

Susan alisema kabla ya kuanza zoezi la kuwarejesha wanyama hao, ulifanyika utafiti kwa kwa wazee wanaoishi karibu na eneo hilo, ambao walibainisha kuwa kulikuwa na wanyama waliokuwa wanaishi katika eneo la Kitulo kabla haijawa hifadhi.

"Wazee wanaoishi karibu na hifadhi hii wamekuwa msaada mkubwa kutokana na kutuwezesha kufanya utafiti kuhusiana na aina ya wanyama waliokuwapo tangu zamani kabla ya eneo hili halijaanza kutumiwa na watu kwa shughuli nyingine," alisema Susan.

Alisema baada ya serikali kutangaza eneo la Kitulo kuwa hifadhi ya Taifa ndipo ulianzishwa mkakati wa kuwarejesha wanyama waliokuwapo ndani ya hifadhi hiyo, na kuwa hadi sasa wamefanikiwa kuwarejesha wanyama aina ya pundamilia na swala ndani ya hifadhi hiyo.

Alisema mbali na kuwarejesha wanyama hao, uongozi wa Hifadhi ya Kitulo una mpango wa kuwarejesha wanyama wengine ambao walikuwa wakiishi katika eneo hilo ambao wanafahamika kama kuro.

"Kuna mnyama kama kuro anatajwa alikuwa anaishi katika eneo hili kwa miaka mingi, kwa hiyo tupo mbioni kumrejesha mnyama huyo katika eneo hili la hifadhi," alisema.

Alisema uwingi wa vivutio vikiwamo maua mazuri, ndege wa aina mbalimbali, maporomoko ya maji na wanyama kutaongeza mvuto zaidi wa watalii hususan watalii wa ndani kutembelea hifadhi hiyo ambayo inafikika kirahisi zaidi muda wowote.

Alisema kuna ushirikiano mzuri kati ya uongozi wa hifadhi hiyo na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi katika kuhakikisha hifadhi hiyo inalindwa na kutunzwa ipasavyo kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.





# Vikao Baraza la Wawakilishi vyazingatia tahadhari corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Raya Issa Mselem, amesema mkutano wa 19 wa Baraza la Wawakilishi unaojadili bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka ujao wa fedha umezingatia tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Mselem aliyasema hayo jana kisiwani hapa, akibainisha kuwa mkutano huo ndiyo kirefu zaidi, ukitarajiwa kuchukua siku 32.

Alizitaja tahadhari zitakazochukuliwa katika mkutano huo kuwa ni pamoja na kufupisha muda wa vikao ambavyo sasa vitafanyika kuanzia asubuhi hadi mchana tu.

Kiongozi huyo wa baraza alisema tahadhari zote zimechukuliwa ikiwamo kuweka vifaa vya kinga dhidi ya ugonjwa wa corona, vifaa vya kupima joto la mwili na vitakasa mikono ambavyo vitawekwa kuanzia nje ya jengo hadi ndani.

Alisema tahadhari nyingine zilizochukuliwa ni baraza kutoruhusu wageni kutembelea shughuli zake wakiwamo wanafunzi au marafiki wa wajumbe kutoka katika majimbo ya uchaguzi'.

"Mkutano wa 19 wa Baraza la Wawakilishi la Tisa umeanza hapa ambapo baraza limechukuwa tahadhari kubwa kwa ajili ya kujilinda na ugonjwa wa corona.

"Tumefupisha muda wa vikao na hakuna wageni watakaotembelea baraza katika kipindi hiki wakiwamo wanafunzi au marafiki na wasaidizi wa waheshimiwa kutoka katika majimbo ya uchaguzi," alisema.

Katika mkutano huo, wizara 16 zitawasilisha makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Kwa mujibu wa ratiba ya mkutano huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, anatarajiwa kuwasilisha bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha Juni 15 mchana baada ya kuwasilishwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar asubuhi.

Ratiba hiyo inaonyesha mjadala wa bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha unatarajiwa kuwa wa siku tatu kisha ukifuatwa na muswada wa sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha hizo.



Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said (wa tatu kulia), akikabidhi msaada wa vyakula na vitu mbalimbali kwa waathirika wa mafuriko wa Ubago Cheche jana, ambapo kaya 200 zimeathirika. **PICHA: MARTIN KABEMBA**.



# Wananchi kugawiwa barakoa bila malipo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma (pichani), amesema barakoa zitakazozalishwa kutokana na fedha zilizotolewa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), zitasambazwa na kugawiwa bure kwa wananchi katika majimbo ya uchaguzi.

Aliyasema hayo jana alipokabidhi jumla ya Sh. milioni 39 kwa viwanda tofauti kwa ajili ya kuzalisha barakoa hizo.

Juma alisema wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka CCM wameamua kufanya hivyo kwa nia ya kuhakikisha wapigakura katika majimbo ya uchaguzi wanakuwa salama dhidi ya maambukizo ya ugonjwa huo.

Alisema Sh. milioni 33 zitapelekwa kwa viwanda vya uzalishaji wa nguo vinavyomilikiwa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Magereza.

Kiongozi huyo pia alisema Sh. milioni tisa zitapelekwa kwa kiwanda binafsi kilichoko Magomeni ambacho kitatengeneza barakoa hizo na kusambazwa kwa wananchi.

# Sababu kesi kuchukua muda mrefu zaanikwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KUCHELEWA kutolewa uamuzi wa dhamana kutoka Mahakama Kuu kumeelezwa kuwa ni moja ya sababu kubwa za kesi hizo kuchelewa kumalizika kwenye mahakama za chini.

Hayo yamebainishwa na Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja, Khamis Ali Simai, alipozungumza na Nipashe ofisini kwake kutokana na kuwapo malalamiko ya kesi nyingi za aina hiyo zinachelewa kutokana na kuwekewa pingamiza za rufani kwa maombi ya dhamana za watuhumiwa.

Alisema mahakama kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka imekuwa na utaratibu mzuri wa uendeshaji wa kesi za aina hiyo, lakini wakati mwingine zinachelewa kutokana na baadhi ya watuhumiwa kukata rufani ya kuomba dhamana Mahakama Kuu.

Khamis alisema katika kesi hizo, watuhumiwa wananyimwa dhamana katika mahakama za mkoa kutokana na uzito na unyeti wa makosa yenyewe, lakini Makahama Kuu inaweza kutoa dhamana kwa sababu madhubuti zinapowasilishwa kwa njia ya maombi ya rufani.

Alizitaja sababu hizo kuwa ni pamoja na mgonjwa ambaye maradhi yake yamethibitishwa na daktari na mwanafunzi.

"Kesi hizi hazina dhamana, lakini wengine huomba Mahakama Kuu, hapa ndipo huchelewa ingawa siyo kesi nyingi," alisema.

Hakimu huyo alisema kesi zimekuwa zikiendeshwa vizuri na wananchi bado wana dhana ile ya zamani ya kwamba kesi zinachelewa.

"Kwa mfano, kesi za 2018 ambazo bado zipo mahakamani mpaka sasa ni 10 na zilizobakia ni za 2019 na 2020 na hizo za 2019 ni zile ambazo zilifunguliwa katika miezi ya Oktoba. Kwa hiyo, kesi hazikai sana," alisema.

Kuhusu vikwazo vinavyomkabili wakati wa usikilizaji wa kesi, hakimu huyo alisema ni kukosekana kwa mashahidi wataalamu kama madaktari na mashahidi wa kawaida.

Alisema ongezeko la kesi za watoto mahakamani linatokana na mmomonyoko wa maadili.

Sababu nyingine ni uwelewa mkubwa kwa wananchi kuripoti kesi hizo tofauti na zamani, akibainisha kuwa wengi waliishia kunyamaza kwa kuhofia aibu.

Mwanasheria kutoka Ofisi ya Mashtaka Zanzibar, Khamis Juma, alisema ucheleweshaji wa kesi upo kwa sababu tofauti ndani ya mahakama.

Alisema kesi ambazo zinazokatiwa rufani kuomba dhamana mahakama kuu, zinachelewa kutolewa hukumu kutokana na mtiririko wa uombaji wa rufani yenyewe na kutatokea kwa mashahidi na hakimu au mwendesha mashtaka kuwa na dharura.

Alisema kuwa kwa zile kesi ambazo zinakuwa zimekatiwa rufani, kuna haja mahakama husika kuwapa elimu wananchi juu ya kuwaeleza hali halisi ya juu ya kuchelewa kusikiliza kesi zao.

Meneja Miradi wa Tamwa Zanzibar, Asha Abdi Makame, alisema kumekuwapo na ucheleweshaji mkubwa wa kesi za udhalilishaji, jambo ambalo linawavunja moyo wananchi.

Alisema kumekuwa na mambo mengi ambayo hurejesha nyuma jitihada za wanaharakati pamoja na wananchi ikiwamo kupangiwa tarehe kortini mara kwa mara bila ya mafanikio.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;109/2020**

Ombi la ABDALAH HUSSEIN ABDALAH Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HUSSEIN ABDALA MWANGOZI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/05/2020.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;106/2020**

Ombi la **SILVESTER WILLIAM MBOMBWE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **WILLIAM MRISHO MBOMBWE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/05/2020.

---

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

MAHAMOUD JAHA SERWED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI T 840 ADC YENYE CHASSIS NO XLEPA4X2Z04267660 NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA TRACTOR YENYE NAMBA ZA USAJILI T488 BJS NA CHASSIS NO 04419817

KWAY OYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
KAH/RB/ 158/2020

---

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI
BILL OF COST NO.16 OF 2019
RICHARD EMMANUEL MOSHI……………APPLICANT
VERSUS
METHOD RICHARD TENGA……………….RESPONDENT

TO: METHOD RICHARD TENGIA
WHEREVER YOU ARE.

NOTICE FOR MENTION

TAKE NOTICE: That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 18th MAY,2020 at 09:00 am before Honorable O.H KINGWELE – DR.

WHEREAS: Service on you has been ordered to be published in the NIPAHSE newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

TAKE FURTHER NORE THAT: In default of non appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
GIVEN UNDER my hand and seal of the Court this 22th day of APRIL,2020.

---

## KUPOTEA KWA KADI

**Ramadhani Kashkash Abdallah** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina TOYOTA BREVIS yenye usajili wa namba T569 DCC iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa :
DAR/KIJ/RB/360449/2020

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;107/2020

Ombi la MUJAHID OMARI JUMA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu OMARI JUMA MGOBOKA.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/05/2020.

157333

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu EMMANUEL ROBERT MWITA anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba T 988CDX, Chassis No.SG5015436 Na Engine No EJ20B599989.

Kwa atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa

KUMB:MWA/NY/RB/359806/2020.

157331

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)

YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;108/2020

Ombi la DANIEL LUGWESA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMIS CHARLES LUGWESA.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/05/2020.

Sahihi ya Hakimu

157330

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ALFRED MINANI ALFRED AMEPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MAZIDA DEMIO LENYE NAMBA ZA USAJILI T916 CUG, INJINI NA. B3000215 NA CHESIS NA. DW3W512396. KADI HIYO ILIKUWA KATIKA BAHASHA ALIYOIPOTEZA AKIWA KITUO KIKUU CHA MABASI BUKOBA.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU AWASILIANE NAYE KWA NAMBA 0621-839852.

AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA RB NA. KAG/BUK/RB/354889/2020.

157328

---

*Kwa Habari*

*Motomoto usikose*

*Gazeti lako la Nipashe kila siku*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# AU kuichunguza dawa ya Madagascar

**ANTANANARIVO,** Madagasca

**Tathimini yake ya dawa ya mitishamba itazingatia maadili ya kiufundi ya kidunia katika kukusanya ushahidi wa kisayansi.**

UMOJA wa Afrika (AU), unafanya mazungumzo na Jamhuri ya Madagascar, ili kupata taarifa za kiufundi kuhusu ufanisi wa dawa ya mitishamba iliyotangazwa inazuwia na kutibu ugonjwa wa virusi vya corona.

Imesema Kamishna wa tume ya AU inayohusika na masuala ya kijamii, Amira ElFadil, alifanya mazungumzo na balozi wa Madagascar nchini Ethiopia, Eric Randrianantoandro, April, 30 na wameafikiana kuwa nchi wanachama watatoa maelezo muhimu muungano wa Afrika kuhusu dawa za mitishamba.

Baada ya kupata maelezo, AU kupitia kituo chake cha udhibiti wa magonjwa - (Africa CDC), kitatathimini taarifa zilizokusanywa kuhusu usalama na ufanisi katika tiba hizo asili dhidi ya virusi vya corona. Dawa hiyo inayohusishwa na mmea wa Kichina unaoitwa Artemisia (pakanga), ambao ni mojawapo ya miti ambayo huchanganywa pamoja na mimea mingine ya Madagascar kama tiba ya ugonjwa wa Malaria.

Africa CDC ni taasisi ya AU inayosaidia nchi wanachama katika juhudi zao za kuimarisha mifumo ya afya na kuboresha uchunguzi, kukabiliana na dharura za magonjwa, kuzuwia na kudhibiti magonjwa.

Hata hivyo, AU imesema kuwa tathimini yake ya dawa ya mitishamba itazingatia maadili ya kiufundi ya kidunia katika kukusanya ushahidi muhimu wa kisayansi kuhusu ufanisi wa mitishamba.

Hatua hii ya AU inakuja baada ya Rais wa Madagascar, Andry Rajoelina, kushiriki kikao cha AU cha wakuu wa nchina kwamba aliwafahamisha wenzake kuhusu dawa ya miti shamba ya Madagascar anayoamini inazuwia na kutibu virusi vya corona.

Hatua hiyo inawadia wakati ambao marais karibu wanne wa Afrika wamesema wanaagiza kiasi kikubwa cha dawa ya mitishamba iliyosemekana kupatikana huko Madagascar kuwa ina uwezo wa kutibu virusi vya corona. **BBC**



Wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza vifaa vya kujikinga na virusi vya corona cha Honeywell, wakimsubiri Rais Donald Trump, alipotembelea kiwanda hicho. **PICHA: REUTERS**

## Kesi ya Jacob Zuma yapigwa kalenda

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

KESI kuhusu ufisadi inayomkabili Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, iliokuwa imepangwa kusikilizwa jana, imeahirishwa hadi Juni 23.

Upande wa mashitaka ulieleza kuwa sababu kuu ya kuhairishwa kwa kesi hiyo ni uwapo wa ugonjwa wa virusi vya corona.

Zuma, mwenye umri wa miaka 78, anashutumiwa kuwa alipokea rushwa kutoka kwa kampuni ya elektroniki na ulinzi Thales katika mkataba wa silaha wenye thamani ya Rand milioni 4, karibu euro 216,000 kwa bei ya sasa, uliyotolewa mwaka 1999.

Zuma na kampuni ya Thales wameendelea kukanusha tuhuma hizo. Mpango wa silaha ulifanyika mwaka 1999 ambao Zuma alihama kutoka mkuu wa jimbo kuwa makamu wa rais. Zuma anashitakiwa kwa kukubali kuchukua malipo yasiyokuwa halali. **RFI**

## Nairobi, Mombasa yafungwa siku moja

**NAIROBI,** Kenya

WAKAZI wa maeneo ya Eastleigh jijini Nairobi na Old town mjini Mombasa nchini Kenya, hawatoruhusiwa kutoka katika maeneo hayo katika kipindi cha wiki mbili zijazo, kuanzia saa moja usiku.

Katazo hilo limeanza kutekelezwa jana na kwamba hakuna raia yoyote aliyeruhusiwa kutoka nje.

Hatua hiyo inalenga kuzuia kuenea kwa maambukizo ya virusi vya corona katika maeneo mengine ya miji ya Nairobi na Mombasa, huku wagonjwa wengine wapya 47 wakitangazwa na kufanya idadi ya maambukizo kufikia watu 580.

Akizungumza na vyombo vya habari, Waziri wa Afya, Mutahi kagwe, alisema kwamba kati ya wagonjwa hao 47, 32 wanatoka Mombasa huku 11 wakitoka Nairobi.

Alisema mtaa wa Bondeni ambao wakazi wake wamekuwa wakikiuka masharti ya afya yaliotolewa na serikali una wagonjwa 18 wapya huku mtaa wa Estleigh ukiripoti wagonjwa watano wapya.

Waziri Kagwe alionya mitaa mingine kwamba itachukuliwa hatua kama hiyo iwapo itaendelea kukiuka maagizo ya Kiafya na kusababisha maambukizo ya kiwango cha juu. Vilevile ameagiza migahawa iliopo katika maeneo hayo iendelee kufungwa wakati wa amri hiyo ya kutotoka nje.

Kagwe alisema kwamba wagonjwa 31 waliogunduliwa na ugonjwa huo ni wanaume huku 16 wakiwa wanawake.

Alisema watu wawili walifariki nyumbani kwao huko Mombasa na kufanya idadi ya waliofariki kufikia 26.

"Iwapo kuna wagonjwa ambao wamefariki nyumbani huko Old Town hiyo inamaanisha kwamba kuna watu wengi wa familia waliopata maambukizo wakiwaangalia wagonjwa hao," alisema Kagwe.

Alisema watu wengine wanane wamepona ugonjwa huo , na kufanya idadi ya wale waliopona kufikia 190. **BBC**

## Masoko ya fedha yaimarika

**LONDON,** Uingereza

BIASHARA kwenye masoko ya fedha duniani imekuwa ikiimarika pole pole wakati serikali zikiondosha masharti ya kutotoka nje yaliowekwa kudhibiti kuenea kwa janga la virusi vya corona.

Wakati huohuo, biashara kwenye masoko ya ulaya ikiwa katika hali ya mchanganyiko.

Kipimo cha hisa cha London (FTSE) kilikuwa chini kwa asilimia 0.4, wakati kile cha Paris CAC-40 na cha Frankfurt DAX biashara yake ilikuwa imeshuka kwa asilimia 0.2.

Masoko ya Asia yalimaliza siku mengi kati yao yakiwa juu Jumatano, wakati kipimo cha hisa cha Hong Kong Hang Seng kikipanda kwa asilimia 1.1.

Kipimo cha Shanghai kilimaliza siku kikiwa juu kwa asilimia 0.6 katika kipindi cha kwanza cha biashara baada ya mapumziko ya muda mrefu. Kipimo cha hisa cha Korea Kusini (KOSPI) kilipanda kwa asilimia 1.7, wakati kile cha Taiwan (TSEC 50) haikuwa na mabadiliko yoyote na ile ya S&P/ASX ilipata hasara ya asilimia 0.4.

Na nchini Marekani biashara kwenye masoko ya fedha kwa vipimo vya Dow Jones, S&P 500 na Nasdaq ilifungwa jana jioni ikiwa imepanda kwa asilimia 0.8. **VOA**

# COURTOIS ASEMA BARCA WASIPEWE UBINGWA




**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois, amesema kwamba, Barcelona hawapaswi kupewa Kombe la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kama msimu hautamalizika na kufutwa.

Barcelona walikuwa wanaongoza kwa pointi mbili kileleni dhidi ya Madrid huku zikiwa zimebakia mechi 11 kumalizika kwa msimu kabla ya kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona Machi mwaka huu.

Kocha wa Barca, Quique Setien anataka msimu huu umalizike, lakini anaamini litakuwa jambo la busara kwa timu yake kupewa ubingwa kama ligi haitaendelea.

Hata hivyo, Courtois hakubaliani na hili akisema kwamba bado kuna safari ndefu kabla ya kupewa taji hilo.

"Walijaribu mara moja dhidi yetu, na wakapoteza mara moja, hivyo tuliwaonyesha wao sisi ni timu bora, lakini wametupita pointi mbili," alisema akiiambia televisheni ya nchini Ubelgiji.

"Hivyo, sikubaliana nae katika hilo. Kwa England, ningeweza kuelewa kwamba, kama Liverpool wangepewa ubingwa. Sijui wana pointi nyingi kiasi gani kileleni.

"Halafu naweza kuelewa kwamba, wanaweza kuwa mabingwa. Lakini kwa upande wetu hapana, bado kuna safari ndefu."

Courtois anaamini kwamba, Madrid bado wana matumaini ya kushinda taji hilo, ambapo kwa mara ya mwisho walishinda msimu wa 2016-17.

# Arteta: Nilikuwa na mwanzo mgumu Arsenal

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alihisi "hakuwa na mawasiliano ya kutosha" ndani ya klabu wakati alipochukua mikoba ya kuinoa Arsenal mwishoni mwa mwaka jana.

Nahodha huyo wa zamani wa Arsenal, Arteta alitajwa kuwa kocha mkuu Desemba mwaka jana akichukua nafasi ya Unai Emery.

Arteta, ambaye aliiongoza Arsenal kushinda mechi nane na sare sita kati ya mechi 16 tangu achukue mikoba kabla ya Ligi Kuu England haijasimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, amesema ilikuwa ngumu kwake kujua wapi anaanzia.

"Kwa kawaida kuja kwenye klabu kwa wakati ule haikuwa rahisi, lakini umetaja neno muhimu ambalo ni nguvu," alisema Arteta katika mahojiano na gwiji wa klabu hiyo, Ian Wright.

"Niliona nguvu ile kwenye mazoezi, na nilijua kwamba tukiingia uwanjani tutakuwa na wakati mzuri kwa sababu nilishawahi kuwa hapa.

"Nilikuwa na bahati kucheza hapa, hivyo kila mmoja alikuwa akionekana yupo nyumbani, lakini hakukuwa na mawasiliano katika maeneo mengi na nikataka kuwaleta wote pamoja.

"Kwanza, nilielewa kwa namna gani nina bahati kuwa hapa halafu nikaweka wazi mtazamo wangu na upande gani tunapaswa kuelekea."

Arsenal walikuwa nafasi ya tisa kwenye msimamo, wakipitwa pointi nane kutoka nafasi ya nne, wakati msimu wa ligi ulipo simamishwa kutokana na milipuko wa ugonjwa wa COVID-19.






# *Martinez aambiwa asisite kujiunga Barca*

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez, ameshauriwa kuirukia haraka nafasi ya kujiunga na Barcelona na kocha wake wa zamani pale Racing, Diego Cocca.

Martinez mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akihusishwa sana na kuwaniwa na Barca akichukuliwa kama mrithi wa muda mrefu wa mshambuliaji, Luis Suarez, ambaye alifikisha umri wa miaka 33 Januari na mkataba wake unamalizika mwakani.

Barca imeripotiwa kutaka kumsajili Martinez kwa kiasi kisichozidi euro milioni 111 ambayo ipo kwenye kipengele cha mkataba wake, huku miamba hao wa Katalunya wakijiandaa kuwauza Ivan Rakitic, Arturo Vidal na Samuel Umtiti ili kupata fedha. Licha ya vipingamizi kadhaa kwenye dili hilo, Cocca, ambaye kwa sasa ni kocha wa Rosario Central, hana shaka kwamba Martinez anatakiwa kuchukua nafasi hiyo ili akacheza na Lionel Messi. Kocha huyo ambaye ndiye alimpa nafasi kwa mara ya kwanza kucheza katika soka la kimataifa Novemba mwaka 2015, ameiambia Sport: "Alinishangaza.

"Kwa namna alivyoonekana amepevuka, alikuwa kama mchezaji aliyecheza kwa kipindi kirefu na mzoefu, alinishangaza sana kwa kiwango chake. "Vijana wengi katika umri ule wanakuwa hawana kasi na kiwango kama alichokionyesha, lakini tangu hapo ameendelea kujiimarisha yeye mwenyewe.

HABARI MICHEZO

# Villas-Boas atoa masharti kubakia Marseille

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Andre Villas-Boas amesisitiza atabakia ndani ya Marseille kama klabu hiyo itaweza kutimiza mahitaji yake.

Kocha huyo wa zamani wa Porto, Chelsea na Tottenham, Villas-Boas alijiunga na Marseille mwanzoni mwa msimu akichukua nafasi ya Rudi Garcia ambaye mafanikio yake ilikuwa tu kuifikisha nafasi ya tano kwenye msimamo.

Kuimarika kwa timu hiyo chini ya Villas-Boas haikuwa kazi rahisi, ambapo ilishinda mechi nne tu katika ya 12 za kwanza kwenye mashindano yote, lakini zikafuatia mechi 16 bila kufungwa.

Ameisaidia timu hiyo kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa nyuma ya Paris Saint-Germain baada ya msimu kufutwa wiki iliyopita.

Lakini Villas-Boas amebainisha kwamba hataendelea kubakia na kikosi hicho kama Marseille hawatakuwa tayari kukamilisha yale anayoyahitaji.

"Katika soka la duniani kuna makocha kadhaa wazuri, sio kwa kumaliza nafasi ya pili kunanifanya niwe kocha bora duniani, au kocha mbaya," alisema akiiambia RMC Sport.

"Nimebakia kama nilivyo. Nilishasema kwenye mkutano wangu na waandishi wa habari kwamba, kama klabu itanitimizia kile ninachokitaka, nitabakia hapa.

"Nataka kufanya usajili. Nataka kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa na Marseille, lakini sijui hali yao kiuchumi."





# HATIMAYE KALOU AOMBA RADHI

**BERLIN,** Ujerumani

BAADA ya kupewa adhabu ya kusimamishwa na klabu yake ya Hertha BSC, Solomon Kalou ameiomba radhi kwa kuvunja sheria ya kuepuka mikusanyiko dhidi ya wachezaji wenzake katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

Kalou aliposti video katika ukurasa wake wa Facebook, ambayo ilimuonyesha akivunja sheria ya kuepuka mikusanyiko, baada ya kumshika mkono mchezaji mwenzake wakati wanafanyiwa vipimo.

Hertha iliamua kumchukulia hatua za kinidhamu kwa kumsimamisha mchezaji huyo raia wa Ivory Coast, kutohudhuria mazoezi na mwendelezo wa baadhi ya michezo ya Bundesliga.

Baada ya adhabu hiyo, Kalou ameamua kuomba radhi kwa kitendo hicho na kwamba alifanya kwa furaha, baada ya majibu ya vipimo kuwa mazuri.

"Samahani kama nilionyesha kutochukulia corona kwa umakini mkubwa, lakini nilifanya vile kuonyesha furaha ya vipimo vyetu," amesema Kalou.

"Naomba radhi kwa wote ambao hawakujua kama nilikuwa najirekodi kwenye video, lakini sikukusudia kujiweka katika hali ambayo imetokea."

# Bruyne bado hajui hatima yake City

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne amebainisha kuwa bado hajui hatima yake ndani ya kikosi hicho kinachotumia uwanja wa Etihad.

City ina mpango wa kumwongezea De Bruyne mkataba mpya ili aendelee kubakia klabuni hapo na asiondoke akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika mwakani.

Lakini wakati City wakitamani mazungumzo yao na De Bruyne yaanze sasa, kiungo huyo amefichua kuwa hana haraka na pia itategemea uwezekano wa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na kocha Pep Guardiola atabaki.

"Bado nafikiri kwamba, Pep ataendelea kubakia hadi mwakani. Nasubiri, lakini uamuzi wangu hautotokana na msimamo wake," alisema De Bruyne.

Manchester City imepanga kumboreshea maslahi kiungo huyo kwa kumlipa mshahara wa pauni 280,000 kwa wiki na kumfanya kuwa nahodha wake.

De Bruyne amekuwa na kiwango bora tangu ajiunge na City mwaka 2015 ambapo ameifungia jumla ya mabao 31 katika jumla ya mechi 143, huku pia akifunga mabao 19 katika mechi 74 za timu ya Taifa ya Ubelgiji.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WILLIAN AKARIBIA KUSAJILIWA SPURS

## Lengo lake ni kuungana tena na Mourinho, lakini familia pia ikichangia kuona...

**LONDON,** England

WINGA wa Chelsea, Willian tayari ameweka wazi anataka kuungana na kocha wake wa zamani, Jose Mourinho kwa kukubali kujiunga na Tottenham katika kipindi cha majira ya joto, beIN Sports ilimeripoti.

**Winga huyo mwenye umri wa miaka 31 anajiandaa kumaliza ngwe yake ya miaka saba ya kukaa katika klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Stamford Bridge wakati mkataba wake utakapomalizika ifikapo Juni, mwaka huu.**

Akizungumza katika kipindi cha Keys & Gray ndani ya kituo cha beIN Sports, Keys alisema kwa kujiamini kuwa: " Mchezaji huyu (Willian) ni nyota mwingine ambaye tayari ameshafanya mazungumo na Jose Mourinho, yuko mbioni kujiunga na Tottenham."

Willian alikiri amefanya mawasiliano na Mourinho na yatakuwa wazi baada ya dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto litakapofunguliwa.

Nyota huyo raia wa Brazili aliwahi kufundishwa na Mourinho ndani ya Stamford Bridge kuanzia Agosti 2013 hadi Desemba, mwaka 2015 kabla ya kocha huyo Mreno hajaondoka klabuni hapo baada ya kufikia makubaliano yaliyosababishwa na kutoelewana, ikiwa ni mara ya pili akikiongoza kikosi hicho.

Lakini Willian aliweka wazi anapenda kuona anaungana tena na Mourinho na kuelezea yeye na familia yake itafurahia zaidi kubakia katika Jiji la London.

Willian aliongeza kuwa bado yeye ni 'rafiki mkubwa' na kocha huyo wa sasa wa Spurs na hana tatizo lolote endapo atajiunga na klabu hiyo pinzani na waajiri wake wa sasa.

Katika mahojiano maalumu na kipindi cha Bolivia Talk Show, Willian alisema: "Hakuna jambo jipya ambalo Mourinho amekuja nalo, lakini sisi wawili tuna mahusiano mazuri na ni rafiki yangu mkubwa.

"Huwa kuna wakati tunazungumza lakini inapofika suala la kuhusu usajili, huwa anaheshimu sana uamuzi wangu."

Willian ambaye anatarajia kumaliza mkataba wa kuitumikia Chelsea katika kipindi cha majira ya joto na alijiunga na klabu hiyo mwaka 2013 akitokea Anzhi Makhachkala.

Hata hivyo ameendelea kusisitiza yeye binafsi na familia yake itafurahi na inataka kuona anabakia London kwa kutokuwa tayari kulihama jiji hilo, lakini bado akiwa hana uhakika ni klabu ipi ataichezea katika msimu ujao.

## ZISIKUPITE

### RAMSEY ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inajiandaa kumsajili kiungo wa Juventus na Timu ya Taifa ya Wales, Aaron Ramsey (29), kama sehemu ya kukamilisha mchakato wa usajili wa kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Express)***

### SPORTING YAPELEKWA FIFA

SPORTING Lisbon imeshtakiwa katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) na Sampdoria, ambayo inadai kutolipwa kiasi cha pauni milioni 4 kama sehemu ya ada ya usajili waliyopata Januari mwaka huu wakati wanamuuza Bruno Fernandes (25), kwa Manchester United. Kiungo huyo Mreno aliondoka Italia na kujiunga na Sporting mwaka 2017. ***(Mirror)***

### ARSENAL KUUZA SITA

ARSENAL italazimika kuuza wachezaji wake sita ili kupata fedha za kusaidia kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Nicolas Pepe (24), ambaye dau lake la kumng'oa Lille katika kipindi cha majira ya joto ni pauni milioni 72. ***(Sun)***

### QUARTA ATAJWA CITY

MANCHESTER City imeonyesha nia ya kumsajili nyota wa River Plate, raia wa Argentina, Lucas Martinez Quarta (23), huku mchezaji mwenzake beki wa kati, Nicolas Otamendi (32), akiwa kwenye mipango kutua River Plate. ***(Sports Witness via TNT Sports - in Spanish)***

### CHIESA AKARIBIA JUVE

JUVENTUS inatarajia kuendelea na mchakato wa kumsajili winga wa Fiorentina na Timu ya Taifa ya Italia, Federico Chiesa, ambaye klabu yake imekuwa kumuuza kwa dau la kawaida. Chelsea, Manchester United na Inter Milan pia zinawania saini ya winga huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Goal)***

### HENDERSON HAKIJAELEWEKA

MANCHESTER United inatakiwa kuchukua uamuzi kuhusu hatima ya golikipa wa Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 21 ya England (U-21), Dean Henderson, ambaye ameonyesha kiwango kizuri alipokuwa kwa mkopo Sheffield United, Mlinda mlango huyo anamaliza mkataba wake na Man United mwezi ujao. ***(Sun)***

### STILLER KUTUA ARSENAL

ARSENAL imeweka wazi nia ya kumsajili kiungo mkabaji wa Bayern Munich, Angelo Stiller, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Bild - in German)***

### MBAPPE AONA MBELE

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe (21), amewaeleza mabosi wake kuweka kipengele kipya katika mkataba wake ambacho kitamruhusu kuondoka na kujiunga na Real Madrid au klabu nyingine ya Ulaya hapo baadaye. ***(AS - in Spanish)***

### TOKO-EKAMBI KUBAKIA LYON

LYON inataka kuhakikisha inambakisha kwa mkopo mshambuliaji wa Villarreal na Timu ya Taifa ya Cameroon, Karl Toko-Ekambi (27). ***(Goal)***

### DC UNITED YASAKA BEKI

DC United bado inasisitiza kufanya mchakato wa kusajili beki wakati dirisha la usajili la Ligi Kuu Marekani litakapofunguliwa, baada ya mipango yake kuvurugika kwa sababu ya kusimamishwa kwa ligi hiyo. ***(MLSsoccer.com)***

## HABARI MICHEZO

## JPM amfurahisha mchezaji wa Lyon

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa African Lyon inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, Jarufu Juma, amesema amefurahishwa na kauli ya Rais, John Pombe Magufuli (pichani) ya kufikiria kuirejesha Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilisimama tangu Machi mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Jarufu alisema amejiandaa kucheza katika kiwango cha juu mara msimu wa 2019/20 utakaporejea tena ili kukitangaza kipaji chake.

Jarufu alisema lengo na ndoto zake ni kusajiliwa na timu yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sababu anaamini uwezo wa kushiriki ligi hiyo anao.



"Ligi ikianza tena nitapambana kwa nguvu zote ili kufikisha mbali timu yangu pamoja na kukitangaza kipaji changu kwa wadau wa soka," alisema Jarufu.

Nyota huyo alisema ametumia vema kipindi chote ambacho ligi zimesimama kufanya mazoezi kwa bidii kwa lengo la kuujenga mwili wake na kurekebisha upungufu uliyokuwa nayo huko nyuma.

"Nashukuru nimepata muda mwingi wa kufanya mazoezi, hata kama ligi ikianza kesho (leo), sina wasiwasi kutokana na maandalizi ya muda mrefu niliyoyafanya," Jarufu alisema.

Aliwataka wachezaji wenzake kuendelea kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona kwa kufuata vema maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

## Mbio za magari mambo magumu

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Mbio za Magari Tanzania (AAT), kimesema endapo serikali itaruhusu michezo kurejea bila mashabiki, kwa upande wao watakuwa na wakati mgumu kwa sababu wataathirika kiuchumi.

Akizungumza na gazeti hili, Msemaji wa AAT, Athuman Khamis, alisema wamesikia kauli ya Rais John Pombe Magufuli juu ya kufikiria kurejesha Ligi Kuu, lakini bado hawana uhakika kama michezo itarejea kama ilivyokuwa awali.

Khamis alisema endapo watarejea katika michezo bila kuruhusu mashabiki, kwao watakuwa na changamoto kwa sababu mashindano yao hufanyika kwa kutegemea wadhamini.

"Tunasubiri mwongozo wa serikali, suala la kutokuwa na mashabiki kwetu ni mtihani, sisi tunapata pesa kwa wale wanaokuja kushuhudia mashindano yetu, ili kusaidia chama kupata fedha za kujiendesha," alisema Khamis.

Alisema endapo utachukuliwa uamuzi wa kutoruhusu mashabiki, AAT italazimika kukutana kujadili hatima ya michuano inayotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

# KMC YAIANGUKIA TFF TAREHE MPYA LIGI KUU

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa KMC FC umeliomba Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutoa muda usiopungua wiki mbili kabla ya kuanza tena kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, ili kusaidia wachezaji kurejea katika muunganiko wa pamoja.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMC FC, Haruna Hererimana, alisema wakipata muda huo, wachezaji wataimarika na kuwa tayari na mapambano kwa kuwa wametoka kwenye mazoezi binafsi bila ya usimamizi wa kocha.**

"Kama Ligi Kuu itaendelea, ninaomba TFF watupe wiki mbili za kuwaandaa wachezaji wetu kwa pamoja, hii itawasaidia kuwaweka sawa kwa sababu wamekaa bila kucheza kwa muda mrefu, wakifanya mazoezi mmoja mmoja," alisema Hererimana.

Kocha huyo alisema siku hizo zinatosha kuwanoa wachezaji wake na kuwafanya warudi kwenye hali ya ushindani kama walivyokuwa kabla ligi haijasimama.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa timu hiyo, Benjamin Sitta, alisema wachezaji wao wanaendelea kufanya mazoezi binafsi ili kujiweka sawa huku wakijikinga na virusi vya ugonjwa wa corona kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

Sitta alisema wanaendelea kujipanga kuhakikisha timu yao inafanya vema katika mechi zilizosalia za msimu huu na huku mradi wao wa ujenzi wa uwanja ukielekea kwenye hatua za mwisho.

"Ujenzi wa uwanja wetu unaendelea vizuri, kama tukishuka daraja tutapata pigo wakati tunahangaika tuwe na uwanja binafsi, ila pia tunatarajia kuziruhusu timu nyingine za hapa jijini na za mikoani kuutumia pale wanapokuwa na mahitaji," alisema Sitta.

Alizitaka timu nyingine zinazomilikiwa na halmashauri mbalimbali kufuata mfano wao na uamuzi huo utasaidia kuongeza miundo mbinu bora hapa nchini.

Ligi Kuu ndio hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati mshindi wa michuano ya Kombe la FA hupeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**MAZOEZI...**



Wachezaji wa Timu ya mpira wa mikono ya Jeshi Stars, wakifanya mazoezi ili kuimarisha viwango vyao kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Alliance yalia mipango imevurugwa*

**Na Saada Akida**

MENEJA wa Alliance FC, James Bwire, amesema janga la maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona limesimamisha mambo mengi ikiwamo mchakato wa kuimarisha timu yao ambayo iko kwenye hatari ya kushuka daraja.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Alliance FC ambayo imecheza mechi 29, iko kwenye nafasi ya 18 ikiwa na pointi 29 ikifuatiwa na Mbao FC yenye pointi 22 na Singida United yenye pointi 15 inaburuza mkia.

Bwire alisema wanashindwa kupanga vema mikakati kuhusiana na mechi zilizosalia na maandalizi ya msimu ujao, kwa sasa hadi jana hakuna tamko rasmi kuhusiana na hatima ya Ligi Kuu Tanzania Bara kutofahamika.

Alisema wanashindwa kupeana majukumu ya kuiandaa timu kwa kukwepa mikusanyiko lakini wakihakikisha wanasaka njia za kutafuta fedha za kuzilipa mishahara ya wachezaji na watumishi wengine wa timu hiyo.

"Kwa sasa tunachokifanya ni kuhimiza benchi la ufundi kuzungumza na wachezaji wetu kuhusu kuzingatia mazoezi wanayowapa, ila kwa upande wa viongozi hatuwezi kusema tunafanya jambo fulani kwa ajili ya kusaidia timu ili ibakie katika ligi," alisema Bwire.

Aliongeza hawajakata tamaa na nafasi waliyonayo wanaweza kujiepusha na janga la kushuka daraja kwa kuendelea kusisitiza makocha wao kuwafuatilia kwa karibu wachezaji.

Alisema pia wanafahamu mechi zilizobakia zitakuwa na ushindani, hivyo kila mchezaji anatakiwa kuwa imara kuisaidia timu yake itimize malengo.

Michezo
Alhamisi Mei 7, 2020
Nipashe




Willian akaribia kusajiliwa Spurs UKURASA 22





Mkurugenzi Mwekezaji wa Kampuni ya GSM ambao ni wadhamini wa Yanga, Hersi Said (kulia), akiwa na mshambuliaji nyota wa timu hiyo Mghana Bernard Morisson. **PICHA: MAKTABA**

## Bundesliga kurejea rasmi mwezi huu

**MUNICH,** Ujerumani

SERIKALI ya Ujerumani imetoa baraka za kurejea kwa Ligi Kuu nchini humo maarufu Bundesliga kuanzia kwa wiki ya pili ya mwezi huu.

Uamuzi huo wa kurejesha Bundesliga umetangazwa katika kikao maalumu kilichofanyika jana Jumatano na kuongozwa na Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel (pichani) pamoja na viongozi 16 wa majimbo ya nchini humo.



Mechi za Bundesliga sasa zinatarajiwa kufanyika kati ya Mei 15 na 22 mwaka huu. Lakini kwanza wachezaji watatakiwa kukaa karantini kwa muda wa wiki moja ili kupunguza uwapo wa maambukizo ya virusi vua ugonjwa wa corona (COVID 19).

Zimebakia raundi tisa ili kukamilika kwa msimu wa 2019/20 wa Bundesliga na michezo hiyo itachezwa bila mashabiki huku watu 322 wakitarajiwa kuhudhuria katika kila mechi huku wakifanyiwa vipimo kila siku.

Ujerumani imetajwa kuwa moja ya nchi za Ulaya iliyofanikiwa katika kuzuia maambukizo mapya ya Covid-19, ambayo kwa siku ya tano mfululizo hadi jana yamefikia idadi ya chini ya watu 1,000.

# Yanga yaandaa mambo mazuri

### Lengo ni kuwa na kikosi 'tishio' ambacho kitatoa 'dozi' mfululizo katika msimu ujao...

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inarejea katika ushindani wa kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Yanga ya jijini Dar es Salaam, umejipanga kuhakikisha unafanya usajili wa vitendo wa nyota wenye viwango vya juu wa kimataifa, imeelezwa.

**Uamuzi huu unatokana na 'hasira' ya kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu miwili mfululizo, huku pia ikipoteza matumaini ya kutwaa taji hilo kwa msimu huu wa 2019/20 ambao unaelekea ukingoni.**

Tayari wadhamini wa Yanga, Kampuni ya GSM, imetangaza kutenga bajeti ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa usajili wa kikosi cha timu hiyo cha msimu ujao kama ilivyopendekezwa na Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael.

Mkurugenzi Mwekezaji wa GSM, Hersi Said, aliliambia gazeti hili kampuni hiyo imejiandaa kufanya usajili wa 'kishindo' kwa ajili ya msimu ujao na mchakato huo utatekelezwa kwa vitendo hivi karibuni.

Said alisema wanataka kuifanya Yanga kuwa timu inayoogopewa katika msimu ujao baada ya GSM kuchelewa kuingia mkataba wa udhamini hapo mwaka jana.

"Tutafanya usajili wa daraja la juu, wa kiwango kikubwa, hii itawashtua wote wanaoiangalia Yanga, usajili wetu utafanywa kwa utulivu kwa sababu tunajua malengo tuliyoyaweka kwa ajili ya msimu ujao," alisema Said. Aliongeza katika kuhakikisha Yanga inapata fedha kupitia mauzo ya jezi za wachezaji wake, wako katika maandalizi ya kuandaa mfumo sahihi kwa kushirikiana ili zoezi hilo liwe na mafanikio.

Kiongozi huyo alisema Yanga, GSM inatarajia kushirikiana na idara za serikali ili kuepusha wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kuingiza nchini jezi feki.

"Tunatengeza mfumo mpya ambao utakuwa unatulinda sisi dhidi ya wale wanaohujumu, tutashirikiana kikamilifu na idara za serikali ili zitusaidie katika jambo hili, tunawakumbusha wanachama kufahamu sehemu sahihi wanazotakiwa kwenda kununua jezi," Said alisema.

Aliongeza wanatarajia kuleta bidhaa zenye ubora wa hali ya juu ambazo zitaongeza chachu ya mauzo kwa ajili ya kusaidia klabu hiyo kupata fedha za kujiendesha.

Ukiondoa wachezaji mbalimbali wa kimataifa wanaotajwa kutua nchini kujiunga na Yanga, nyota wa hapa nchini walioko kwenye rada za timu hiyo ni pamoja na mshambuliaji wa Namungo FC, Relliants Lusajo na beki wa kushoto wa Polisi Tanzania, Yassin Mohamed.

"Tangu nilipoanza kusikia tetesi za uongozi kutaka kumsajili Lusajo na Yassin, nimekuwa nikiunga mkono kwa asilimia zote, kwani ni wachezaji wazuri, Lusajo tulishawahi kuwa naye Yanga, hivyo anaifahamu vizuri changamoto zake, ila hata hivyo utaona Yanga ilimwacha si kwa ubaya isipokuwa kocha wa kipindi hicho alikuwa na mastraika wengi, Yassin yeye nilianza kumkubali tangu alipokuwa Ndanda FC, hivyo naujua uwezo wake," Nahodha Msaidizi wa Yanga, Juma Abdul alisema.

Hata hivyo, bado Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), halijafungua rasmi dirisha la usajili na sasa linaendelea na vikao mbalimbali ili kujua hatima ya Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na mashindano ya Kombe la FA ambayo yalisimamishwa ili kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042